Leo yetu ndiyo kesho yetu

# Uelekeo



Kigali tayari kimewaka

Uk. 24

| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00029 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Septemba 13 - 19, 2023 |

# Rais Samia ang'ara anga za kimataifa

- **Ateuliwa Mjumbe wa Bodi ya Taasisi kubwa duniani**

Uk. 4



Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Kituo cha Dunia cha Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi (GCA), Katibu Mkuu Mstaafu wa Umoja wa Mataifa, Ban Ki-moon, alipowakilisha taarifa ya uteuzi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, wakati wakizungumza pembezoni mwa mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika jijini Nairobi, Kenya wiki iliyopita. Picha: Ikulu



KIMATAIFA

Uk. 19

## Miili 44 ajali ya moto bado haijatambuliwa

HABARI

Uk. 8

## TPA yaahidi makubwa Mtwara





MAKALA

Uk. 16

## Teknolojia yavuta vijana kwenye ujenzi

## 1,397,370 waanza mitihani kuhitimu elimu ya msingi

Uk. 4

NECTA inatoa wito kwa wasimamizi wote walioteuliwa kusimamia mitihani kufanya kazi yao ya usimamizi kwa makini na uadilifu wa hali ya juu...





## Halmashauri zote kupewa magari matatu ya wagonjwa

Uk. 3

# Mawaziri watatu kwa mpigo wammwagia sifa Dk. Samia

**Na Claudia Kayombo, Iramba**

MAWAZIRI watatu wa Serikali ya Awamu ya Sita, Wamemwagia sifa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kuwa ni kiongozi wa mfano katika utekelezaji wa miradi mbalimbali inayoharakisha maendelea endelevu nchini.

Kwa msingi huo, mawaziri hao wamewataka wananchi waendelee kumunga mkono Rais Dk. Samia.

Mawaziri hao ni Waziri wa Ujenzi, Inocenti Bashungwa, Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba na Waziri wa Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo.

Walimmwagia sifa hizo wakati wa hafla ya makabidhiano na Meneja wa Kampuni ya Henan Highway Engineering Group ya China, Huang lele, inayotarajiwa kuanza kujenga mradi wa barabara yenye urefu wa kilomita 77.6 kutoka Sabasaba hadi Kizaga.

Hafla hiyo ilifanyika eneo la Misigiri katika Jimbo la Iramba Magharibi ambapo mgeni rasmi alikuwa ni Waziri wa Ujenzi Bashungwa ambaye alisema kuanza kwa ujenzi wa barabara hiyo, kunatokana na Rais Dk. Samia kutambua na kuthamini kazi za kiuchumi zinazofanywa na wananchi wa mkoani Singida.

Alisema kukamilika kwa barabara hiyo pamoja na mambo Mengine, kutachochea uchumi kwa wana-Singida na taifa kwa jumla.

Aliwaomba wananchi kuonesha ushirikiano kwa mkandarasi atayeanza kujenga barabara hiyo kwa kulinda vifaa vya ujenzi na kumpa ushirikiano atakaouhitaji ili kukamilisha kazi hiyo kwa wakati.

Kwa upande wake, Waziri Fedha, Dk. Nchemba baada ya kuwashukuru wananchi kwa kuhudhuria hafla hiyo, alisema alipogombea ubunge kwa mara ya kwanza mwaka 2010, aliwaahidi atajenga barabara hiyo, lakini alikuwa anapambana bila mafanikio katika tawala zilizopita.

Hata hivyo, alisema katika utawala wa Serikali ya Awamu ya Sita, alipodokeza tu hilo kwa Rais Dk. Samia, amekubali mara moja na muda mfupi ujayo itaanza kujengwa.

Naye Waziri wa Mipango na Uwekezaji, Dk. Mkumbo alisema Rais Dk. Samia anafanya kazi nzuri kwa wakazi wa Singida ikiwamo teuzi za viongozi mbalimbali wa juu kutoka mkoa huo.

Alisema hatua hiyo inaonesha mapenzi makubwa aliyo nayo kwao hivyo zawadi pekee wanayoweza kumpa ni kura katika uchaguzi mkuu ujao.

Meneja wa Kampuni ya Henan Highway Engineering Group ya China, Huang Lele, pamoja na mambo mengine, aliomba ushirikiano miongoni mwa wananchi wa Singida kuwezesha kukamilisha ujenzi huo kwa wakati.



# Askari wamnasua mtoto wa tembo

**Na Beatus Maganja, TAWA**

ASKARI wa Hifadhi kutoka Mamlaka ya Usimamizi Wanyamapori Tanzania (TAWA), wamefanikiwa kumuokoa mtoto wa tembo anayekadiriwa kuwa na umri wa wiki nne aliyezama katika shimo lenye matope katika Kijiji cha Kwamsanja kilichopo Kata ya Kibindu Halmashauri ya Chalinze jirani na Pori la Akiba Wami Mbiki mkoani Pwani.

Taarifa za mtoto huyo wa tembo aliyetelekezwa na kundi la wenzake baada ya kutumbukia shimoni, zilitolewa na raia mwema, Manase Baha, mkazi wa Kijiji cha Kwamsanja.

Hali hiyo ilimlazimu Kamanda wa Pori la Akiba Wami Mbiki, Emmanuel Lalashe, kutuma timu ya askari wanne walioshirikiana na askari sita wa Jeshi la Akiba (mgambo) ambao walifanikiwa kumuokoa.

Akizungumza baada ya uokoaji huo, Kamanda Lalashe aliwashukuru wananchi wanaoishi pembezoni mwa pori hilo kwa ushirikiano wanaoutoa katika kulinda rasilimali za taifa zilizopo katika hifadhi hiyo wakiwamo wanyamapori ambao ni chachu ya shughuli za utalii na Pato la Taifa.

Taarifa hiyo ilisema mahusiano mazuri yaliyojengwa kati ya Wahifadhi wa Pori la Wami Mbiki na wananchi wanaoishi vijiji jirani na pori hilo, umekuwa na manufaa makubwa siku za hivi karibuni kwani wananchi wamekuwa wakitoa ushirikiano mkubwa katika shughuli za uhifadhi.







# CCM: Madiwani simamieni miradi kikamilifu

**Na Allan Vicent, Sikonge**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) wilayani Sikonge, kimewataka madiwani wa Halmashauri ya wilaya hiyo, kuhakikisha miradi inayotekelezwa na serikali inasimamiwa ipasavyo ili kuleta tija kwa wananchi.

Katibu wa CCM Wilaya ya Sikonge, Magdalena Ndwete, aliagizo hilo alipokuwa akitoa salamu za Chama katika kikao cha kufunga mwaka cha Baraza la Madiwani.

Alisema serikali imepeleka fedha nyingi katika halmashauri hiyo kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika sekta za elimu, afya, maji, barabara na nishati, hivyo ni jukumu la madiwani kuhakikisha fedha hizo zinafanya kazi iliyokusudiwa.

Alisema baadhi ya wakandarasi wamekuwa wakichelewesha miradi pasipo sababu yoyote, hivyo akaagiza kila diwani kufuatilia fedha zinazotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi katika kata yake na kutoa taarifa haraka anapoona kazi haifanyiki.

'Madiwani simamieni kwa dhati utekelezaji miradi ya maendeleo, serikali inatoa fedha nyingi sana ili miradi ya wananchi ikamilike kwa wakati, lakini cha kusikitisha baadhi ya maeneo miradi inasuasua na diwani yupo,' alisema.

Aidha, aliwataka kufuatilia utekelezaji wa maazimio yote yanayotolewa katika vikao vya baraza hilo ili kuleta tija kubwa kwa maendeleo ya jamii ikiwemo kutatua kero za wananchi.

Mkuu wa wilaya hiyo, Simon Chacha, aliipongeza halmashauri hiyo kwa kufanikiwa kukusanya zaidi ya asilimia 92 ya mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani, huku akiwataka kuweka mikakati zaidi ili kutimiza malengo yao kwa asilimia 100.

Aliwakumbusha kuwa halmashauri haiwezi kufanikisha utekelezaji mipango yake ya maendeleo kama haina mapato ya kutosha, hivyo akawataka madiwani, watendaji wa vijiji na kata na Ofisi ya Mkurugenzi, kuongeza ubunifu katika hilo.

Vile vile, alimtaka Mkurugenzi kuwachukulia hatua stahiki watendaji au mtumishi yeyote atakayetafuna fedha za mapato au kutowasilisha makusanyo yake kwa wakati ili kukomesha tabia hiyo.

# Kila halmashauri kupewa magari matatu ya wagonjwa

**Na Mwandishi Wetu, Songwe**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema serikali imeagiza kila halmashauri nchini kupewa magari matatu ya kubebea wagonjwa na yatumike kwa ajili ya huduma za dharura na rufaa.

Alisema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, aliagiza serikali kuzipatia halmashauri magari mawili na wizara yake kutoa gari moja.

Alitoa kauli hiyo juzi mkoani Songwe wakati akizungumza na madaktari, wauguzi na timu ya usimamizi wa Halmashauri ya Wilaya ya Songwe, katika ziara yake mkoani humo.

"Mtapatiwa magari matatu ya kubebea wagonjwa ili kusaidia kutoa huduma za dharura na rufaa za matibabu na kupunguza madhara makubwa yanayoweza kusababisha vifo kwa wagonjwa wanaohitaji huduma hizo kwa haraka," alisema na kuongeza:

"Magari haya yatasaidia kupunguza vifo vya mama na mtoto, lakini pia kurahisisha mgonjwa kupata huduma kwa haraka pale anapopatiwa rufaa au anapohitaji huduma za dharura," alisema.

Hata hivyo, aliwasisitiza wananchi wa halmashauri hiyo kujitokeza kupeleka watoto katika kupata chanjo dhidi ya ugonjwa wa polio inayotarajiwa kuanzia Septemba 21 mpaka24, mwaka huu ili watoto wao waweze kupata chanjo ya ugonjwa huo.

"Baada ya kupatikana kwa mgonjwa mmoja mwenye ugonjwa wa polio mkoani Rukwa, Wizara ya Afya tumeamua kutoa chanjo hiyo kwa mikoa sita ikiwemo Mkoa wa Rukwa, Kagera, Kigoma, Mbeya, Katavi na Songwe, hivyo ninawaomba sana wazazi kushiriki kwa kuwatoa watoto," alisema.

Aidha, aliiagiza Bohari Kuu ya Dawa nchini (MSD) kuhakikisha upatikanaji wa vifaa tiba katika halmashauri hiyo ili Hospitali ya Wilaya ya Songwe ili ianze kutoa huduma katika sehemu ambazo hazijaanza.

"Naiagiza MSD hakikisheni vifaa tiba vinapatikana kwa wakati na mvigawe katika Vituo vya Afya ikiwamo wilaya hii ili huduma zipatikane hasa katika huduma za mama na mtoto," alisema Waziri Ummy.



**Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo amekutan na Balozi wa Jamhuri ya Kishoshalisti ya Vietnam nchini Tanzania, Nguyen Nam Tien, kwa ajili ya mazungumzo katika Ofisi Ndogo ya Makao Makuu ya CCM, Mtaa wa Lumumba, jijini Dar es Salaam jana. Balozi huyo alifika ofisini hapo kwa ajili ya kumuaga Katibu Mkuu Chongolo, baada ya kumaliza muda wa kuiwakilish nchi yake Tanzania.**

# Uzalishaji wa maji tiba sasa wafikia chupa 720 kwa siku



**Na Mwandishi Wetu**

HOSPITLI ya Rufaa ya Kanda ya Bugando mkoani Mwanza, imekamilisha ukarabati wa kiwanda cha kuzalisha maji tiba kitakachokuwa na uwezo wa kuzalisha chupa 720 kwa siku.

Awali, kiwanda hicho kilichokuwa kinazalisha aina zaidi ya 10 za maji tiba, kilikuwa kinazalisha chupa 400 kwa siku huku uboreshwaji huo ukiongeza uzalishaji wa maji hayo kwa matumizi ya ndani hadi kufikia asilimia 93.

Akizungumza kwenye makabidhiano na uzinduzi wa kiwanda hicho juzi, Mfamasia katika Kitengo cha Maji Tiba Bugando, Deus Sinibagiye, alisema uboreshaji wa kiwanda hicho ni endelevu huku akidokeza kuwa Kitengo cha Maji Tiba kina lengo la kuongeza uzalishaji wa maji hayo hadi chupa 1,400 kwa siku.

"Kiwanda hiki kimeipunguzia taasisi gharama ya ununuzi wa maji tiba kwani sasa hivi hapa Bugando, chupa moja inatengenezwa kwa gharama isiyozidi Sh. 650 ambapo bei ya sokoni kama tungeenda kununua, ni kati ya Sh. 850 na Sh. 1,000," alisema.

"Maboresho haya yamesaidia kupunguza gharama ya upatikanaji wa maji hayo ambapo Agosti kitengo kilifanikiwa kuokoa zaidi ya Sh. milioni 20 kutoka kwenye chupa 10,000 zilizotumika mwezi uliopita," alisema.

Naye, Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Bugando, Dk. Fabian Massaga, aliwaomba wadau wenye nia ya kuwekeza katika uzalishaji wa maji tiba, kuchangamkia fursa hiyo ambayo alisema lengo ni kutanua wigo na kuzalisha kwa ziada ili kusambaza kwenye hospitali nyingine za Kanda ya Ziwa.

"Tutaendelea kuboresha miundombinu ya uzalishaji wa maji tiba na vifaa tiba ili kuleta utoshelevu katika huduma zinazotolewa kwa wagonjwa. Huu ni utekelezaji wa ushauri uliotolewa na wataalam wa Mamlaka ya Chakula na Vifaa Tiba (TMDA) walipotembelea hospitali yetu," alisema.

Dk. Massaga aliwataka wataalam na watumishi wa hospitali hiyo kutunza kiwanda hicho sambamba na kuzingatia weledi wanapozalisha ili kulinda afya za wagonjwa na watumiaji wa maji hayo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Huduma za Afya Saidizi Bugando, Dk. Cosmas Mbulwa, alisema hospitali hiyo inapambana kuongeza mtaalam mmoja ili wafike wanane kuwezesha uzalishaji ufanyike mara mbili kwa siku.

# Samia ang'ara kimataifa

## ● Ateuliwa Mjumbe wa Bodi ya Taasisi kubwa duniani

**Na Hellen Mwango**

NYOTA ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, imeng'ara kimataifa baada ya kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Bodi ya Ushauri ya Kituo cha Dunia cha Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi (GCA).

Taarifa ya uteuzi huo iliwasilishwa na Mwenyekiti wa GCA ambaye ni Katibu Mkuu Mstaafu wa Umoja wa Mataifa, Ban Ki-moon wakati akizungumza na Rais Dk. Samia pembezoni mwa mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu mabadiliko ya tabianchi uliofanyika jijini Nairobi, Kenya hivi karibuni.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu Chamwino, jijini Dodoma, Zuhura Yunus, heshima hiyo ni utambuzi wa uongozi mahiri wa Rais Dk. Samia, katika jitihada za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi Afrika na duniani kote ambako Tanzania ni kinara kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali barani Afrika.

Taarifa hiyo iliwataja Wajumbe wengine wa bodi hiyo kuwa ni Rais wa Jamhuri ya Senegal, Macky Sal, Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika, Moussa Mahamat, Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AFDB), Akinumwi Adesina na Mkurugenzi Mwendeshaji wa Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF), Kristalina Geogieva.

GCA ni taasisi kubwa duniani inayosimamia masuala ya uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi na kwamba hadi sasa inaweza kufanikisha upatikanaji wa zaidi ya Dola za Marekani bilioni 50 huku Tanzania ikiwa miongoni mwa nchi za kwanza zitakazonufaika katika kipindi cha miaka mitatu ijayo.



# 1,397,370 waanza mitihani kuhitimu elimu ya msingi

**Hellen Mwango na Godfrey Sanga**

BARAZA la Mitihani la Tanzania (NECTA), limesema wanafunzi 1,397,370 wa darasa la saba kutoka shule aa msingi 18,320, leo wanaanza mitihani ya kuhitimu elimu ya msingi.

Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Said Mohamed, aliyasema hayo katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jijini Dar es Salaam jana kuwa watahiniwa hao watafanya mitihani ya masomo ya Kiswahili, Kingereza, Sayansi na Teknolojia, Hisabati, Maarifa ya Jamii, Stadi za Kazi na Uraia na watamaliza kesho.

Alisema idadi hiyo ya watahiniwa, inajumuisha wavulana 654,652 sawa na asilimia 46.85 na wasichana 742,718 sawa na asilimia 53.15.

Alisema kati ya watahiniwa hao, 1,334,269 watafanya mtihani kwa lugha ya Kingereza ambayo wamekuwa wakiitumia katika kujifunza.

Kwa upande wa watahiniwa wenye mahitaji maalum, alisema wapo 4,583 ambao kati yao 101 ni wasioona, 1,321 wenye uoni hafifu, 1,125 wenye uziwi, 549 wenye ulemavu wa akili na 1,487 ni wenye ulemavu wa viungo.

Alisema mtihani wa kumaliza elimu ya msingi, ni muhimu kwa wanafunzi na jamii kwa ujumla kwa kuwa hupima maarifa na umahiri wa wanafunzi katika masomo waliyosoma katika elimu ya msingi.

Alisema matokeo ya mtihani huu, hutumika katika uchaguzi wa wanafunzi wanaojiunga katika elimu ya sekondari, hivyo ni mtihani muhimu wa wanafunzi, wazazi na jamaii nzima katika Taifa.

"Maandalizi yote kwa ajili ya mtihani huo kwa idadi ya watahiniwa niliyoitaja yamekamilika ikiwamo kusambazwa kwa makaratasi ya mtihani pamoja na nyaraka zote muhimu zinazohusu mtihani huo katika Halmashauri/Manispaa zote nchini, maandalizi yote kwa ajili ya watahiniwa wenye mahitaji maalumu yamefanyika ipasavyo.

"Kamati za mitihani za Mikoa na Halmashauri zimefanya maandalizi yote muhimu kwa kutoa semina kwa wasimamizi wa mtihani pamoja kuhakikisha kuwa mazingira ya vituo vya mtihani yapo salama, tulivu na kuzuia mianya yote inayoweza kusababisha kutokea kwa udanganyifu," alisema.

Alifafanua kuwa pamoja na maandalizi yote muhimu yaliyofanyika, Kamati za Mitihani za Mikoa na Halmashauri, zihakikishe kuwa usalama wa vituo vyote vya mtihani unaimarishwa na kwamba vituo hivyo vinatumika kwa kuzingatia mwongozo uliotolewa na NECTA.

"NECTA inatoa wito kwa wasimamizi wote walioteuliwa kusimamia mitihani kufanya kazi yao ya usimamizi kwa makini na uadilifu wa hali ya juu, wahakikishe kuwa wanafanya kazi ya usimamizi wa mtihani huo kwa weledi na kwamba na kwa kuzingatia kanuni za mitihani na miongozo waliopewa ili kila mtahiniwa apate haki yake na wahakikishe wathaniwa wote wanafanya mtihani kwa muda uliopangwa na katika hali ya utulivu.

"Watahiniwa wenye mahitaji maalum, waongezewe muda wa dakika 20 kwa kila saa kwa somo la Hisabati na dakika 10 kwa masomo mengine kama mwongozo wa NECTA unavyosema," alisema.

Aidha, aliwataka wananchi wote watoe ushirikiano katika kudhibiti vitendo vyovyote vya udanganyifu katika mtihani huo, Baraza halitasita kumchukulia hatua yeyote atakayebainika kujihusisha au kusababisha udanganyifu wa mitihani kufanyika kwa mujibu wa sheria za nchi.

Pia wadau wote wanaombwa kutoa taarifa katika vyombo husika kila wanapobaini uwepo wa mtu au kikundi cha watu kujihusisha na udanganyifu wa mitihani wa aina yoyote taarifa ziwasilishwe moja kwa moja NECTA.

**NECTA inatoa wito kwa wasimamizi wote walioteuliwa kusimamia mitihani kufanya kazi yao ya usimamizi kwa makini na uadilifu wa hali ya juu, wahakikishe kuwa wanafanya kazi ya usimamizi wa mtihani huo kwa weledi**







# TIRDO yaanika faida lukuki za makumbi ya

**Na Hellen Mwango**

SHIRIKA la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO), limesema utafiti umebaini faida kubwa ya makumbi ya nazi kama vile kutengenezea nyavu za uvuvi, vitanda na kamba imara zinazohimili maji ya chumvi bila kuoza kwa muda mrefu.

Kauli hiyo ilitolewa jijini Dar es Salaam na Mtaalamu wa Utafiti wa Ngozi na Nguo wa TIRDO, Bosco Mtweve wakati akizungumza na Uelekeo ofisini kwake.

"Tumezoea kuvuna mafuta kutoka kwenye nazi kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, lakini makumbi yake yana faida kubwa…sisi tunayachakata na kuzalisha kamba za kutengenezea nyavu za uvuvi, vitanda na matumizi mengine kwa kuwa ni imara sana, haziozi wala kuchakaa haraka," alisema.

## Hakimu atoa hofu madai ya kesi za kubambikiwa

**Na Eunice Lugiana, Pwani**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Kibaha mkoani Pwani, imewatoa hofu wananchi kuhusu suala zima la kubambikiwa kesi kwa kuwa zikifikishwa mahakamani, haki hutendeka kwa wakati.

Kauli hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi wa mahakama hiyo, Fahamu Kibona, wakati akizungumza na wananchi waliokwenda mahakamani hapo juzi kupata huduma .

Hakimu Mkazi Kibona alisema:"Huwezi kuthibitisha kesi ya kutengeneza kwa kuwapanga mashahidi watano wote waseme uongo unaofanana, lazima watajichanganya tu."

Alisema tofauti iliyopo kati ya kesi za madai huangaliwa mizani uzito ulipo, lakini kwa kesi za jinai zinatakiwa kuthibitishwa pasipo kuacha shaka na pia lazima kuwepo na nia ovu ya kutenda kosa hilo.

Aliwatoa shaka wananchi hao kuwa hisia haziwezi kusasabisha mtu kutiwa hatiani isipokuwa ushahidi uliothibitika pasipo kuacha shaka ndiyo humtia mtu hatiani.

Aidha, Hakimu Kibona akitoa elimu kwa wakazi hao katika ukumbi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kibaha, alitolea mfano kwamba, ng'ombe aliyekuwa amefungwa kamba na mfugaji, lakini akakata kamba na kwenda kwenye shamba na kuharibu mazao, hiyo haiwezi kuwa jinai kwa sababu hakuna nia ovu maana yeye alimfunga, lakini akakata kamba na kwenda kuharibu mazao bila mfugaji kujua.

Aliongeza kuwa katika tukio kama hilo, haiwezi kuwa kesi ya jinai maana hakuna nia ovu ya mfugaji kuruhusu ng'ombe wake kwenda kuharibu mazao, moja kwa moja katika kisa hicho aliyeharibiwa mazao anapaswa kufungua kesi ya madai badala ya jinai.

Akitoa mfano wa kesi ya Chacha Mginga iliyotokea zamani na kuandikwa katika vitabu vya mkusanyiko wa kesi mbalimbali, Hakimu Kibona alisema Mahakama ilimhukumu mshtakiwa kwa kosa la kuua bila kukusudia, maana mshtakiwa hakukuwa na nia ovu ya kuua.

Kwa mujibu Hakimu huyo, mshtakiwa alikuwa anawinda nyani wasiharibu mazao yake akakuta watu wawili usiku shambani wakifanya mapenzi na kwa kuwa ilikuwa usiku ilibidi aulize mara tatu kama ni watu au la, lakini hakupata jibu, basi kwa mawazo yake alitarajia kama ni watu watajibu, lakini kwa kukaa kimya, alijua hao nyani, hivyo, ndipo alifyatulia mshale uliomuua mmoja wao.

Mtuhumiwa alishtakiwa kwa kosa la mauaji ya kukusudia, lakini kutokana na ushahidi, ilionekana aliua bila kukusudia.

Akijibu swali lililoulizwa na mwananchi ambaye jina lake hakutaka litajwe kuhusu kumhisi mtu kumbambikia kesi, Hakimu Kibona alieleza kuwa hisia haziwezi kumtia mtu hatiani isipokuwa ushahidi uliothibitika bila kuacha shaka ndiyo utamtia mtu hatiani.

Aidha, Hakimu Kibona aliongeza si kweli kwamba hakimu hufurahia kusoma hukumu ya kumfunga mtu, bali hutimiza wajibu wake wa kutoa haki bila kupendelea upande wowote.

Alifafanua kuwa mahakama inabeba asilimia 50 za upande wa mshtakiwa na asilimia 50 za upande wa Jamhuri, hivyo anakaa pale kama muamuzi kwa yule atakayethibitisha.

## Kesi tuhuma kujipatia mil. 20/- kuanza kunguruma Oktoba 3

**Emeryciana Deus na Aisha Ramadhan TUDARCo**

KESI ya kujipatia Sh. milioni 20 kinyume cha sheria inayowakabili Abdallah Mashaka (57) na Felix Amoni (73), katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam, itaanza kusikilizwa Oktoba 3, mwaka huu.

Upande wa Mashitaka katika kesi hiyo ulidai kuwa mshtakiwa Mashaka alimdanganya Guardian Simon, kuwa anaitwa Iddi Selemani Kisesa na kufanikiwa kumuuzia kiwanja kilichopo eneo la Tabata Kisukuru eneo la Bonyokwa, kwa thamani ya Sh. milioni 20.

Akisoma hoja za awali, Wakili wa Serikali, Winnie Samson, alidai kuwa Julai 27, mwaska 2018 na Septemba 18, mwaka 2018 maeneo ya Tabata Kisukuru Bonyokwa, mshtakiwa Mashaka alimdanganya Simon kuwa anaitwa Iddi Seleman Kisesa.

Alidai kuwa Felix Amon, aliwahi kuwa Mjumbe wa Shina Tabata Kisukuru Bonyokwa na yeye ndiye aliyemtambulisha Abdallah Mashaka kama Iddi Seleman Kisesa na kumuaminisha mnunuzi kuwa ndiye mmiliki wa eneo hilo.

Alidai kuwa mshtakiwa Mashaka alijipatia kiasi cha Sh milioni 20 kwa njia ya udanganyifu baada ya kumuuzia Simon kiwanja kilichopo eneo la Tabata Kisukuru Bonyokwa huku akijua kufanya hivyo ni kosa kisheria.

Alidai kuwa malipo hayo yalifanyika mbele ya mshtakiwa Amon ambaye alimwaminisha mnunuzi huyo kuwa eneo hilo ni mali ya Mashaka, jambo ambalo halikuiwa la kweli.

Baada ya maelezo hayo, Hakimu aliahirisha kesi hiyo hadi Oktoba 3, mwaka huu kwa usikilizwaji.

# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi


## HII NI KERO

### Kuombaomba barabarani



SUALA la kuwa ombaomba hasa kwa kukaa kando kando ya barabara, limekuwa kero kwa watu wengi, ingawa kiuhalisia, wapo wenye shida dhahiri ambao wanahitaji msaada. Je; kila mtu mwenye maisha magumu anapaswa kuomba msaada mtaani?

Idara ya Ustawi wa Jamii inapaswa kutengeneza utaratibu stahiki ili kuwabaini wenye uhitaji na kuwawezesha kwa lengo la kuwaepuka matapeli.




## MAONI YA MHARIRI

# Kila la kheri darasa la saba, ila jiepusheni na udanganyifu

BARAZA la Taifa la Mitihani (NECTA), jana lilitangaza kuanza kwa mitihani ya kuhitimu elimu ya msingi kwa mwaka 2023.

Kwa mujibu wa NECTA, jumla ya wanafunzi 1,397,370 wa darasa la saba kutoka shule aa msingi 18,320, ndiyo wanatarajia kufanya mitihani hiyo.

Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Said Mohamed, alitangaza hayo kupitia vyombo vya habari jijini Dar es Salaam jana.

Kwa mujibu wa Dk. Mohamed, watahiniwa hao watafanya mitihani ya masomo ya Kiswahili, Kingereza, Sayansi na Teknolojia, Hisabati, Maarifa ya Jamii, Stadi za Kazi na Uraia na kuhitimisha kesho Alhamisi.

Aidha, alisema kati ya watahiniwa hao, wavulana 654,652 sawa na asilimia 46.85 na wasichana 742,718 sawa na asilimia 53.15.

UELEKEO tunawatakia kila kheri wanafunzi hao na kuwataka waitumie vema fursa hiyo kwani haijirudi tena.

Baadhi ya wanafunzi wamekuwa wakifanya 'madudu' kwenye mitihani hiyo pasipo kuelewa kuwa hiyo ni moja ya hatua kubwa katika maisha yao.

Mnapaswa kuelewa kuwa mitihani hiyo ni kipimo chenu cha uelewa katika miaka yote saba mliyokuwa mkisoma tena baadhi yenu na wazazi wenu wenye vipato vya chini.

Lakini pamoja na kuwatakia kila la kheri na kuwapa ushauri huo, tunawaomba mjiepushe na janja janja yoyote ya udanganyifu wa mitihani kwani kwa kufanya hivyo, mtakuwa mmepoteza bure muda wenu wa miaka saba shuleni.

Udanganyifu kwenye mitihani iwe kwa darasa la saba, kidato cha nne na hata wa kidago cha sita, ni tatizo ambalo hujitokeza karibu kila mwaka.

Sote tu mashahidi adhabu ambazo huwakumba wote wanaobainika kufanya udanganyifu huo.

UELEKEO tunawashauri darasa la saba wote wa mwaka huu, muachane kabisa na mchezo huo mchafu, kwani muelewe kuwa mnapofanya udanganyifu, matokeo yake Taifa litapata wataalam wa fani mbalimbali wakiwemo madaktari, marubani, walimu, wanasayansi ambao ni `vilaza.'

Je, Taifa linapopata wataalamu wa namna hiyo, matokeo yake yatakuwa ni nini?

Msidanganywe na mtu, kikundi ama kundi lolote la kutaka kuwapeleka huko, tumieni uwezo wenu mliofundishwa na walimu wenu kufanya mitihani na tunaamini nyote mtafanya vizuri.

Kila kheri na tunawatakia mitihani mema.

## Wasiliana nasi


**Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000
**Mhariri wa Habari:** +255753333330
**Mhariri Michezo:** +255787559090
**Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825
**S. L. P:** 15110, Dar es Salaam
**Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro
**Jengo la:** Aura Mall
**Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532
**Email:** uelekeohabari@gmail.com




Na Valensi Mbaga
JICHO LANGU
Valeyjames24@gmail.com

# Awamu ya sita kumaliza kero ya foleni barabarani

MAZURI ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ni mfano wa kuigwa kwa namna unavyoacha alama chanya katika maendeleo ya uchumi wa nchi.

Jicho langu siku ya leo limelenga hasa Wizara ya Ujenzi ambayo Innocent Bashungwa, ni Waziri wake.

Wizara hii inayofanya mambo makubwa kutokana na maboresho mbalimbali yaliyofanyika, hususan ujenzi wa barabara stahiki, madaraja, reli, viwanja vya ndege, bandari na kadha wa kadha, hivyo kurahisisha mawasiliano kati ya mkoa na mkoa, wilaya na wilaya na hivyo kukuza uchumi wana nchi kwa kasi.

Serikali ya Awamu ya Sita ikisimamia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020-2025 kupitia ibara ya 54 (b), (c), (d), ibara ya 55 (e) na (f), na ibara ya (57) (f) ya ilani hiyo imeielekeza serikali kuondoa msongamano wa magari na kuboresha huduma za usafiri wa umma Dar es Salaam na miji mingine mikubwa ya Tanzania.

Kupitia msingi huo, serikali imetekeleza miradi mbalimbali katika maeneo mbali mbali ya jiji la Dar es Salaam ili kuondoa foleni na kuboresha miundombinu.

Azma ya serikali kutekeleza sera hiyo imesababisha miradi mbalimbali ikiwemo mradi wa barabara ya Mwenge-Morocco ambao tayari umekamilika na hivyo kuondoa adha ya foleni katika barabara hiyo.

Pili mradi wa ujenzi wa barabara za mitaa kwa kiwango cha lami katika viunga vya eneo la Gerezani (Kariakoo) unatajwa kuwa utaondoa foleni na kurahisisha mawasiliano katika eneo hilo ambapo mwanzo palikuwa na miundombinu mibovu ya barabara na kupelekea kuwa na ugumu wa huduma katika maeneo hayo.

Lakini pia serikali imefanikiwa kutekeleza mradi wa stendi iliyopo Mwenge (Dar es Salaam) ambayo itakwenda kutatua adha ya kukosekana kwa stendi inayopelekea usumbufu na foleni kubwa katika eneo hilo kutokana na uegeshaji mbovu wa daladala mradi huu umekamilika kwa zaidi ya asilimia 75.

Serikali haijaishia tu katika eneo moja kwani kuna miradi mikubwa na ya kihistoria ya kujenga barabara ndefu kwa wakati mmoja, ikiwemo ujenzi wa barabara zenye urefu wa zaidi ya kilomita 1780 nchi nzima na katika maeneo mbalimbali ya nchi miradi hii imesaidia sana sekta nzima ya usafirshaji na mawasiliano.

> **Serikali haijaishia tu katika eneo moja kwani kuna miradi mikubwa na ya kihistoria ya kujenga barabara ndefu kwa wakati mmoja, ikiwemo ujenzi wa barabara zenye urefu wa zaidi ya kilomita 1780 nchi nzima.**

Baadhi ya miradi hiyo ni ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami yenye urefu wa kilomita (438) kutokea Arusha – Kongwa, ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutokea Tabora –Koga-Mpanda ambayo imeshakamilika kwa zaidi ya asilimia 82.

Ujenzi wa madaraja mbalimbali ikiwemo Tanzanite Bridge, Wami Bridge pamoja na viunga vyake ambayo yote yameshakamilika na yanatoa huduma stahiki kwa umma.

Ninukuu kwa kusema, "mzazi hawezi kumuacha mwana akaungua na kiazi kilichotoka mikononi mwake," kumaanisha kwamba Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, hawezi kuwaacha wananchi wateseke katika nchi ambayo anaiongoza yeye mwenyewe.

# Huduma za wawekezaji kupatikana sehemu moja

**Na Mwandishi Wetu**

KITUO cha Uwekezaji nchini (TIC) mwishoni mwa wiki hii, kitazindua mfumo wa kielektroniki wa kuhudumia wawekezaji mahali pamoja ujulikanao kama Tanzania Investment Electronic Window.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Kaimu Mkurugenzi wa Kituo hicho, John Mnali, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uzinduzi huo.

Mnali alisema uzinduzi huo utafanyika kesho kutwa na mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Alisema mfumo huo umetokana na kuunganishwa kwa mifumo mbalimbali ya taasisi za serikali ambazo zinahusika na kutoa vibali na leseni kwa wawekezaji.

Taasisi hizo zimeunganisha mifumo yao ambayo inatumika kusajili wawekezaji na kutoa vibali na kwamba kwa awamu ya kwanza utaunganisha taasisi saba.

Alisema mfumo huo utaunganisha Wakala wa Usajili wa Leseni na Biashara Brela, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), TIC kwa ajili ya utoaji wa leseni na vyeti vya uwekezaji, Kamishna wa Kazi kwa ajili ya vibali vya kazi, Uhamiaji kwa ajili ya vibali vya kazi.

Alitaja taasisi nyingine ni Wakala wa Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Wizara ya Ardhi kwa ajili ya ardhi kwa wawekezaji wa kigeni.

"Kwa awamu hii, mwekezaji atakuwa anaingia kwenye mfumo mmoja atakapoanza usajili wa kampuni ataendelea na kuomba vibali mbalimbali kupitia mfumo huo na taarifa zake za awali ambazo mwekezaji atakuwa amezitoa kama jina lake, jina la kampuni, wamiliki wa kampuni taarifa hizo zitapatikana kwenye taasisi zote za serikali bila kulazimika kutoa taarifa hizo kila wakati," alisema.


Mnali alisema mfumo huo utamrahisishia mwekezaji kupata vibali na leseni mbalimbali ndani ya muda mfupi tofauti na ilivyokuwa kabla ya mfumo huo.

Alisema kupitia uzinduzi huo, wanatarajia pia kuzindua mwongozo utakaotumiwa na watoa huduma kwa wawekezaji kwani baadhi yao huomba huduma ya usajili wakiwa nje ya nchi.

"Kuna wakati, mwekezaji yuko nje ya nchi na anataka kusajili kampuni au kupata leseni kwa hiyo siku ya uzinduzi wa dirisha la pamoja pia tutazindua mwongozo wa watu hawa wanaotoa huduma hizi kwa wawekezaji hii huduma tunaita Investors Service Providers Guidelines," alisema

Alisema watazindua kampeni maalum ya kuhamasisha uwekezaji wa ndani na wa nje ili kupata wawekezaji wengi zaidi wa ndani na kutoka mataifa mengine watakaowekeza kwenye miradi mbalimbali.

"Tumetengeneza kampeni maalum ya kuvutia ambayo inaonyesha program mbalimbali za kuvutia uwekezaji kwenye mikoa mbalimbali ili wawekezaji wa nje na wazawa waje kuwekeza na kwa kweli uzinduzi wa tools hizi tatu, utasaidia kwa kiwango kikubwa kuvutia uwekezaji," alisema.



Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, akizungumza na watumishi wa Manispaa ya Musoma mkoani Mara (hawapo pichani), wakati wa ziara ya kukagua utekelezaji wa Mpango wa Kuondoa Umaskini nchini (Tasaf) jana.

Picha: Mpigapicha Wetu

# Wajasirimali mkaa mbadala wajengewa uwezo

**Na Hellen Mwango**

ZAIDI ya wajasiriamali wa uzalishaji 100 wa mkaa mbadala, wamepata mafunzo ya kuwajengea uwezo wa uzalishaji bora na wa kisasa kutoka Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO).

Hatua hiyo imelenga kuendeleza harakati za utekelezaji wa agizo la Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, la kutumia nishati safi ifikapo mwaka 2030.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkurugenzi Mkuu wa TIRDO, Profesa Mkumbukwa Mtambo, wakati akifungua mafunzo ya wajasiriamali wa mkaa mbadala (biomass briquettes) kama nishati safi kwa matumizi ya majumbani, taasisi na hata viwandani jijini Dar es Salaam jana.

"Mafunzo haya tumeshirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kupunguza Umaskini (Repoa) katika kuwajengea uwezo wajasiriamali wanaozalisha mkaa mbadala nchini ili kuunga mkono lengo la Serikali inayoongozwa na Rais Dk. Samia kwa Watanzania kutumia nishati safi ifikapo 2030, natumaini kila mmoja wenu ana shauku kama mimi ya kushiriki mafunzo haya muhimu kwa ustawi wa uchumi, mazingira na afya zetu," alisema.

Alisema mkaa mbadala ni bora katika kutunza mazingira, TIRDO kwa kushirikiana na Repoa ambaye ni mshiriki mwenza katika utafiti huo uliowezesha uboreshaji wa uzalishaji wa mkaa mbadala wa bayomasi, wameandaa mafunzo hayo ili kuwalisha kile walichotafiti sasa kikafanye kazi kwa wajasiriamali.

Aidha, alisema mafunzo hayo ya siku tatu, yametayarishwa baada ya kufanya utafiti uliofanywa na TIRDO kwa kushirikiana na Repoa katika mikoa 12 (asilimia 39) hapa nchini na kutembelea wazalishaji mkaa mbadala 58 na watumiaji 122, ukiwa na lengo la 'kuimarisha uzalishaji wa mkaa mbadala na kukuza matumizi yake kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi nchini.

"Juhudi hizi zimefanywa ili kukidhi lengo tajwa hapo juu na kuendana sambamba na tamko la Rais (pamoja na Mwongozo wa nchi uliotayarishwa) la kuwa na nishati safi ya kupikia mpaka ifikapo mwaka 2030," alisema Profesa Mtambo.

Naye Mkurugenzi Mkuu Repoa, Dk. Donald Mmari, alisema wameandaa mafunzo hayo ili kuwawezesha wajasiriamali kufanya uzalishaji salama na bora bila kuwasababishia madhara ya kiafya na kuongeza uzalishaji wenye tija na kutosheleza mahitaji katika jamii.

Pia, alisema matumizi ya mkaa mbadala una mchango mkubwa wa kutunza mazingira kutokana na malighafi zinazotumika ikiwamo vifuu vya nazi na maganda ya matunda mbalimbali.

"Baada ya mafunzo haya natoa wito kwa taasisi binafsi kuwawezesha wajasiriamali mitaji ili waweze kukuza na kuongeza uzalishaji wa nishati hiyo kwa kiwango kikubwa ikiwamo kutumia mashine za kisasa zenye kuwaweza salama kwa afya zao," alisema Dk. Mmari.

Alisema Dk. Samia alishatoa agizo taasisi zinazohusika na kusimamia na kutoa vibali wasiweke vikwazo ili kuwachelewesha wajasiriamali kukuza mitaji yao.

Kwa upande wake, mjasiriamali kutoka Mkata mkoani Tanga, Abdulkheri Kesi alisema, serikali isimamie tamko lake kuhakikisha taasisi ikiwamo vyuo kuanza kutumia mkaa mbadala ili kuwaongezea ajira wananchi.

Alisema kiwanda chake kimeajiri wafanyakazi wa kudumu 24 kati yao wanawake ni 18 na vibarua wanane hivyo, soko likiongezeka ajira zitaongezeka na kukuza uchumi wa pato la taifa.

# CCM Singida yawafunda wabunge, madiwani

**Na Claudia Kayombo, Singida**

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Singida, Martha Mlata, amewataka wabunge na madiwani mkoani hapa, kuweka mikutano ya hadhara kuelezea kiasi cha fedha zinazotolewa na serikali na namna zinavyotekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Martha alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki wakati akihutubia kwenye hafla ya kumkabidhi mradi wa ujenzi wa barabara ya Sabasaba, Sepuka, Ndago hadi Kizaga yenye urefu wa kilomita 77.6 Meneja wa Kampuni ya Henan Highway Engineering Group ya China.

Ujenzi wa barabara hiyo utagharimu zaidi ya Sh. bilioni 88.

Madiwani na wabunge wote wa mkoa huu, muige hiki alichokifanya Waziri Mwigulu Nchemba, mkawaeleze wananchi fedha zinazotolewa na Mama zinavyotumika," alisema Martha akiwa eneo la Misigiri Jimbo la Iramba Magharibi ilikofanyika hafla hiyo.

Mwenyeki huyo wa CCM Mkoa wa Singida alisema kukamilika kwa ujenzi wa barabara hiyo, kutafungua fursa nyingi za kiuchumi kwa wananchi wa mkoa huu.

Aidha, aliwataka wananchi mkoani hapa, kutambua jitihada za utendaji kazi zinazofanywa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Hata hivyo, Martha alitumia fursa hiyo kuwaombea ajira ndogondogo vijana na kinamama mkoani hapa kwa Waziri Bashungwa wakati wa ujenzi wa barabara hiyo.

"Mgeni rasmi (Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa), naomba ajira ndogondogo wapewe vijana wetu pamoja na kinamama popote mradi huu unapopita," alisema Martha.

Aliwashukuru viongozi wa dini waliohudhuria hafla hiyo na wengine kote nchini kwa kuliweka taifa mikononi mwa Mungu, hatua inayosaidia kudumisha amani nchini.

# TPA yaahidi makubwa Bandari ya Mtwara



**Na Mwandishi Wetu, Mtwara**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), imeahidi kuimarisha utendaji wake na kuwahakikishia wateja na wadau wa Bandari ya Mtwara kuwa bandari hiyo sasa ipo tayari kuhudumia shehena zote kwa asilimia 100 zikiwamo za korosho kutokana na kupatikana kwa makasha ya kutosha na meli za uhakika za kusafirisha shehena hizo.

Naibu Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Mhandisi Juma Kijavara, aliyasema hayo wiki iliyopita kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Plasdus Mbossa, wakati wa maadhimisho ya wiki ya mamlaka hiyo ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha miaka 18 tangu kuanzishwa kwake 2005.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Kanali Ahmed Abbas, alisema katika kuunga mkono juhudi za kazi inayotekelezwa kwa vitendo na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Alisema TPA kupitia Bandari ya Mtwara, imevuka lengo lililolewekwa la kuhudumia tani 400,000 na kufikisha jumla ya tani milioni 1 kwa mwaka.

Alisema anaipongeza TPA Mtwara kwa kuvuka lengo kwa mwaka 2022/23 ni vyema kuwa inaongeza ufanisi hivyo kuifanya bandari hiyo kushika nafasi ya pili kwa uzalishaji baada ya Bandari ya Dar es Salaam.

"Napongeza jitihada za TPA katika kupanua huduma zake ambapo katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 inatarajia kuanza ujenzi wa bandari maalum ya kuhudumia mzigo mchafu katika eneo la Kisiwa Mgao mkoani Mtwara... Serikali ya mkoa wangu inajivunia uwepo wa bandari hii kutokana na ushirikiano mkubwa inaoupata katika shughuli mbalimbali za kuunga mkono juhudi za wananchi za kujiletea maendeleo," alisema.

Naye Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Ligula, Mkoa wa Mtwara, Dk. Lobikieki Kissambu anaishukuru mamlaka hiyo kwa msaada wa vifaa tiba vya Mama na Mtoto, ikiwamo vitanda 15 vya kujifungulia wajawazito pamoja na vifaa muhimu (Delivery Kit with self sterlilization) 10 ili kuongeza uwezo wa hospitali hiyo kutoa huduma bora kwa wanawake wenye uhitaji huo, vikiwa na thamani ya Sh. milioni 30.

Mamlaka hiyo imeweka kipaumbele cha kusaidia huduma za Afya, Elimu na Miradi mbalimbali ya maendeleo ya wananchi na jamii.

Mbali na Mtwara, maadhimisho kama hayo yamefanyika katika makao makuu ya Bandari za Tanga, Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika ikiwa ni kiashiria cha nia njema ya TPA kushirikiana na wananchi katika kuimarisha huduma za kibandari kote nchini sambamba na kulinda miundombinu ya bandari kwa

# Watakiwa kuchangamkia kozi zitolewazo na Veta

**Na Claudia Kayombo, Singida**

WATANZANIA hususan wakazi wa Mkoa wa Singida, wametakiwa kuchangamkia kozi fupi zinatolewa na Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) Singida, kwa kuwa zinawapa fursa ya kuajiriwa au kujiajiri.

Mratibu wa kozi fupi na uzalishaji wa chuo hicho, Sylvester Ndallah, aliyasema hayo jana wakati akizungumzia faida ya kozi hizo kwa Watanzania walio wengi bila kujali umri wao.

"Wanaoweza kusoma kozi hizo ni wahitimu kuanzia elimu ya msingi hadi vyuo, lakini pia walioko kazini kama madereva au wajasirimali wengine wanaotaka kupanua ujuzi na kwa hakika wengi waliozisoma wamejikomboa kiuchumi," alisema Ndallah.

Alifafanua kuwa kozi hizo hutolewa kuanzia wiki mbili hadi miezi ita, wahitimu hupata fursa ya kujiajiri au kuajiriwa serikalini au katika taasisi binafsi.

Alisema mitaala ya kozi fupi inampa fursa yeyote kujifunza ujuzi wa aina mbalimbali unatolewa na chuo hicho nan kuwataka Watanzania hususan wenye ndoto za kujikwamua kiuchumi kupitia ujasiriamali kwa maana ya ufugaji na ujuzi mwingine, kwenda kujiunga na chuo hicho.

Ndallah alizitaja kozi zinazotolewa na chuo hicho kuwa ni ufugaji wa wanyama, ushonaji nguo, ufundi umeme, ufundi bomba, ufundi uchomeleaji vyuma, ufundi magari, useremala, ujenzi, kompyuta, udereva, mapambo, upishi na uhazili.

Mratibu huyo alisema kozi fupi zinawafaa pia walioko kazini mfano madereva ambao wanataka kuongeza ujuzi.

"Tuna kozi ya udereva wa kujihami hii tunawafundisha madereva katika kipindi cha wiki mbili hadi tatu, hapa hujifunza namna ya kuchukua tahadhari wawapo barabarani,"alifafanua na kuongeza:

"Pia tunatoa kozi fupi kwa madereva wa magari ya mizigo, mabasi makubwa yanayokwenda mikoani na nchi jirani."

# Kortini kwa kuchoma miti iliyopandwa na DC Mbeya

**Na Zawadi Kapambwe, Mbeya**

JOSEPH Gaya (37), mkazi wa jijini Mbeya, amefikishwa katika Mahakama ya Mwanzo Mjini Mbeya kujibu shitaka la kuchoma moto miti yenye thamani ya Sh.300,000.

Akitoa ushahidi wake, mlalamikaji ambaye ni Mwanasheria wa Serikali, Ladislaus Kisandu, alidai kuwa siku ya tukio, mshtakiwa alichoma miti 30 iliyopandwa na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya.

"Mheshimiwa Hakimu, serikali kila kukicha inahamasisha kupanda miti kwa wingi ili tupate hewa safi na mvua kwa wingi ...halafu anakuja mtu mmoja asiyejielewa na kuchoma miti 30 iliyopandwa na Mkuu wetu wa Wilaya, hilo haliwezekani lazima sheria ifuate mkondo ili iwe fundisho kwa wengine wenye lengo la kutaka kutenda kosa hilo,"alidai wakili huyo.

Naye Afisa Misitu wa jijini Mbeya, Gema Revokatus, alidai kuwa kazi yake ni kusimamia misitu na kupanda miti na kwamba anao uzoefu wa miaka minane katika kazi yake hiyo.

Afisa huyo alitoa ushahidi wake mahakamani hapo kuwa siku ya tukio alipigiwa simu na wakazi wa eneo hilo kuwa mshtakiwa ndiye aliyechoma moto miti.

Alidai, alidai kuwa siku ya kupanda miti hiyo wakiwa kazini na jopo la wafanyakazi katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, walikwenda kwenye vyanzo vya maji lililopo eneo la Mwashari jijini hapa na kupanda miti 250 aina ya mzambarau na miembe pori.

Hata hivyo, alidai kuwa baada ya kuipanda miti hiyo, mshtakiwa aliyekuwa akilima hapo, aliichoma moto na kuipulizia dawa kali ya kuikausha ambapo miti 30 ilikauka hapo hapo na mingine kuendelea kunyauka taratibu.

Mshtakiwa alifikishwa mbele ya Hakimu Mfawidhi wa mahakama hiyo, Asha Njovu, ambapo alitenda kosa hilo Januari, mwaka huu eneo la Mwashari jijini Mbeya.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Septemba 20, mwaka huu itakapotajwa tena, ambapo mstakiwa atatoa utetezi wake.

Jarida hili haliuzwi

*Leo ndiyo, kesho yetu*

Uelekeo

JARIDA
# Jungu kuu

| Jumatano Septemba 13 - 19, 2023 |




# Rais Samia anavyozidi kuipaisha TIRDO



UK. 12 & 13

UK. 10

UK. 16

Afya

# Faida za ulaji dagaa kiafya usizozijua

**Na Godfrey Sanga kwa msaada wa mtandao**

WATU wengi huchukuliwa dagaa hutumika kama mboga kwa watu wa kipato cha chini ama cha wastani. Hata hivyo, hii ni dhana potofu kwsani ukweli ni kwamba kitoweo hicho kina manufaa makubwa kwa afya ya kila mwanadamu kama makala hii inavyoeleza.

Dagaa ni zao la baharini, maziwa ama mtoni ni miongoni mwa chakula maarufu duniani.

Kwa ukanda wa Afrika Mashariki, ni kitoweo maarufu na mara nyingi kutumiwa kama mboga ya kula na wali ama ugali japo wapo wanaoitumia kama sehemu ya kichocheo cha ladha wakati wa mlo wowote hata kama wakati wa kifungua kinywa.

Kuna aina nyingi za dagaa, kuanzia wanaotoka baharini hadi ziwani. Wataalamu wa lishe kutoka maeneo mbalimbali duniani wamekuwa na lugha zinazofanana na kutueleza kuwa dagaa ni nzuri zenye faida lukuki tofauti na inavyodhaniwa na wengi.

## Faida za ulaji dagaa

Kwa mujibu wa wataalamu, dagaa hujulikana kama pilchards. Ni samaki wadogo wenye mafuta ambao ni wa familia moja kwa asili na anchovies. Wanaweza kununuliwa wabichi, waliohifadhiwa kwa kukaangwa au jua kwenye makopo au mifuko laini.

Dagaa wanaweza kuwa na umbo dogo, lakini huongeza sana faida kwa chakula licha ya udogo wake, kwa kuwa ni chini ya mafuta yaliyojaa kalori, lakini juu ya protini. Pia hutajwa kuongeza safu nzuri ya vitamini na madini, kama ifuatavyo:-

**Sehemu ya 100 gram ya dagaa safi iliyopikwa:**

- 72 kalori 25.4 gram
- protini 7.8 gram ya mafuta
- 496 miligaram potasiamu
- 63 miligram ya kalsiamu
- 5 gram vitamini D
- 12 miligram ya niasini
- 0 gram vitamini B12
- 65gram selenium
- 101 gram ya iodine

Dagaa za makopo ni mbadala mzuri kwa mbichi au zilizokaushwa na zinapatikana zikiwa zimehifadhiwa kwa mafuta ya aina tofauti, kama vile mafuta ya mizeituni, brine na mchuzi wa nyanya.

### Faida gani kuu za kiafya za dagaa

**1. Kinga ya moyo**

Dagaa labda inajulikana zaidi kwa kuwa samaki wa mafuta na kwa hiyo ni chanzo kizuri cha asidi ya mafuta ya Omega-3, asidi muhimu ya mafuta ambayo mwili lazima upate kutoka kwa chakula kwani hauwezi kuifanya yenyewe.

Asidi ya mafuta ya Omega-3 kwa asili ni ya kuzuia uchochezi na kinga ya moyo kwani imegundulika kuwa na athari nzuri dhidi ya atherosclerosis, shinikizo la damu na thrombosis.

**2. Husaidia afya nzuri ya akili**

Asidi ya mafuta ya Omega-3 pia imegunduliwa kusaidia afya njema ya akili kwa kuzuia hali kama vile wasiwasi na mfadhaiko na kusaidia kuongeza viboreshaji muhimu vya neurotransmitters (kemikali za ubongo) katika ubongo pamoja na serotonin.

**3. Husaidia kutengeneza seli nyekundu za damu**



Vitamini B12 inayotoka kwenye dagaa ina jukumu muhimu katika utengenezaji wa seli nyekundu za damu ambazo husaidia kusafirisha oksijeni kuzunguka mwili.

**4. Husaidia afya ya mifupa**

Dagaa, ni chanzo kizuri cha kalsiamu, huimarisha mifupa laini ambayo inaweza kuliwa. Kalsiamu ina jukumu muhimu katika afya ya mfupa na dagaa inaweza kufanya nyongeza nzuri kwa lishe yako ikiwa ni mjamzito au hutumii bidhaa za maziwa.

**5. Husaidia kudhibiti uzito**

Kutokana na kiwango kikubwa cha protini, dagaa husaidia kukuwezesha kushiba kwa muda mrefu na kupunguza matamanio ya sukari, ambayo inaweza kusaidia kupunguza uzito kiafya au kudhibiti uzito.

Protini ndiyo nyenzo ya ujenzi kwa misuli yako, kwa hivyo dagaa pia ni nyongeza nzuri kwa lishe yako ikiwa unatafuta kuongeza uzito wa misuli.



Utalii



# Sifa, uwezo na maisha ya ngiri

**Na Godfrey Sanga kwa msaada wa mtandao**

NGIRI ni mnyama ambaye wengi wamekuwa wakimfananisha na wakimwita nguruwe pori, ukweli ni kwamba ngiri na nguruwe pori, ni wanyama wawili tofauti.

Licha ya kuvutia kwao na kufanana kwa mbali, lakini ni muhimu kujua kina sifa, uwezo na maisha ya ngiri.

Sifa na tabia ya ngiri

I. Wana sura bapa na pua zilizochongoka zaidi ambao hufanana na za nguruwe.

II. Macho ya ngiri yapo sehemu ya juu zaidi kichwani na huwa hawana uwezo wa kuona mbali zaidi. Macho kuwa sehemu ya juu ya kichwa humsaidia ngiri kumuona adui hata kama kainamisha kichwa wakati wa kula.

III. Wana jozi mbili za viungo ambazo huonekana chini ya macho na katikati ya macho na meno yaliyochomoza, lakini dume huwa na ongezeko la jozi moja ambayo huonekana kwa chini ya taya.

IV. Wana meno yaliyotokeza nje ambayo yapo manne, mawili yapo kwa pembeni mwa pua na yenye umbo la nusu duara na mawili mengine yapo kwa upande wa chini ambayo hutumika sana kwa kukatia vitu.

V. Wana manyoya mafupi sana mwilini, japo sehemu ya juu kichwani kuelekea mgongoni wana manyoya mengi kidogo ukilinganisha na sehemu nyingine za mwili.

VI. Ngozi zao zina rangi ya kijivu au nyeusi lakini anapokuwa ameingia kwenye tope basi huonekana akiwa na rangi ya manjano inayoshabihiana na wekundu.

VII. Wana mikia myembamba na mirefu kidogo. Pindi wanapokimbia, mikia husimama juu mithili ya bendera na hasa kwa watoto hali ya kusimamisha mikia ni kama ishara ya wao kukimbia pamoja na uelekeo mmoja.

VIII. Mara nyingi hukimbia mwendo wa kawaida na unaweza kuwadharau lakini ukweli kwamba wana uwezo wa kukimbia kwa kasi tena kubwa tu ambayo hufika kilometa 48 kwa saa.

IX. Wanapenda sana kuogelea kwenye maji lakini hata mchanga pia kwani inawasaidia kuondoa wadudu katika miili yao.

X. Madume huishi peke yao na hukutana na majike wakati wanapotaka kuzaliana tu. Hali kadhalika majike huishi pamoja na kundi moja linaweza kuwa na kina mama hadi 40.

XI. Hupumzika na kulala maeneo yenye mashimo na hasa maeneo yenye majani ili kupata joto. Japo wana uwezo wa kuchimba mashimo, ngiri huwa hawapendi kuchimba na mara nyingi hutumia mashimo yaliyochimbwa na wanyama wengine kama mhanga.

XII. Wakati mwingine anapokuwa na hasira huamua kushambulia na yeye badala ya kujificha dhidi ya maadui zake.

XIII. Kama walivyo nguruwe, ngiri pia hawana matezi ya jasho mwilini na hupunguza joto mwilini kwa kuoga kwenye matope au maji safi.

XIV. Ngiri wa kawaida wana meno ya mbele mawili juu na manne hadi sita kwenye taya ya chini na hii ni moja kati ya tofauti kati ya ngiri wa kawaida na ngiri wa jangwani kwani hawana meno haya.

XV. Wana uwezo mkubwa sana wa kunusa na kusikia.

Kimo, urefu na uzito

Kimo - ngiri hufikia kimo cha futi 2.1-2.8, urefu - hufikia urefu wa futi 3, uzito - ngiri hufikia uzito wa kilogramu 54 hadi 113.

Mazingira

Ngiri hawa wanapendelea maeneo yenye majani ya savanna yenye miti miti, wanapenda kukaa kwenye mashimo ambayo huwa yanachimbwa na wanyama wengine japo huwa hawagombanii au kumfukuza mnyama mwenye shimo lake. Wao huenda kwenye mashimo ambayo tayari yameshaachwa na wanyama wengine.

Chakula

Ngiri ni jamii ya wanyama walao majani na wanapo kula huwa wanapiga magoti. Wakati mwingine hutumia pua na meno kuchimba mizizi pamoja na baadhi ya mimea ambayo huifadhi chakula ndani ya ardhi.

Wakati wa ukame hasa panapokuwa hakuna majani ya kutosha ngiri hulazimika kula nyama japo huwa hawawindi. Hivyo hulazimika kula mizoga ambayo imeachwa na wanyama wawindao.

Hupendelea kunywa maji mara kwa mara kama walivyo wanyama wengine walao majani.

Kuzaliana

Kama tulivyoona hapo awali, madume na majike hukutana wakati wa kuzaliana tu na baada ya hapo kila kundi huenda njia yake. Mara baada ya kupandana jike hukaa na mimba kwa muda wa miezi sita na kuzaa watoto hadi wanane japo mara nyingi huzaa watoto wanne.

Watoto wa ngiri huzaliwa wakiwa na uzito mdogo sana ambapo hukadiriwa kuwa na uzito wa gramu 450 hadi 900. Kila mtoto huwa na chuchu yake ya kunyonya kwa mama na hata kama imetokea mtoto mmoja kafa basi chuchu yake haitanyonywa na wenzie na itabaki hivyo mpaka mama atakapo zaa tena. Japo watoto hunyonya kwa takribani miezi minne, ila mara tu baada ya miezi miwili tangu kuzaliwa watoto hupata lishe nyingi kupitia majani wanayokula.

Ngiri huanza kuzaliana mara afikipo miezi 20 tangu kuzaliwa. Na wakati huu majike hubaki na kundi la kina mama wakati watoto wa kiume hufukuzwa kisha kwenda kuungana na wenzao na hutengeneza kundi lao.

Maisha ya ngiri hasa katika mazingira asilia huwa ni miaka 12 hadi 18.

Uhifadhi

Kwa mujibu wa shirika linalohusika na uhifadhi wa maumbile asili duniani (IUCN) bado halijawaweka wanyama hawa kwenye kundi la wanyama walio hatarini kutoweka na hii ni kwa sababu wanyama hawa bado wameendelea kutawanyika na kupatikana maeneo mengi sana katika mazingira yao.

Hivyo ni faraja kubwa sana kuona bado wanyama hawa wanaendelea kuwepo tena kwa idadi nzuri na yenye kuridhisha kwa kweli.

Maadui zao

Maadui wakubwa wa ngiri ni simba na chui. Mara ngiri anapohisi kuna hatari au kumuona simba ama chui huamua kukimbia na endapo kuna shimo karibu basi huingia ndani ya shimo huku akitanguliza sehemu ya nyuma.

Tishio kubwa kwa wanyama hawa ni ujangili katika maeneo ya hifadhi za wanyamapori. Hii inatokana na kuongezeka kwa mahitaji na biashara ya nyamapori miongoni mwa jamii mbalimbali kitu kinachosababisha wanyama hawa kuwindwa sana.

Bila kusahau uharibifu wa mazingira na uvamizi wa watu katika maeneo ya wanyamapori. Watu wamekuwa wakiharibu sana mazingira na kuvamia maeneo ya hifadhi za wanyamapori kisha kuanzisha makazi maeneo hayo. Hali hii inasababisha mabadiliko ya kiikolojia na mabadiliko ya kitabia kwa wanyama hawa.

HITIMISHO

Tunaposema tuwatunze wanyapori wetu basi kweli tuwe na nia ya kutekeleza hilo kwa kuanzia ngazi ya jamii hadi mamlaka husika. Hawa ngiri ambao leo tunawaona ni wengi tusipokuwa makini nao watapungua kama walivyo tembo na faru kwa sasa na hata simba pia.

Uvamizi wa maeneo ya hifadhi za wanyamapori ni tatizo kubwa sana hasa kwa ngiri hawa. Ukiangalia pale Hifadhi ya Taifa ya Saadani, ngiri na mifugo ya kawaida wanaishi pamoja kabisa bila matatizo. Hili ni tatizo kubwa sana kwani hapa tayari kuna mabadiliko ya kitabia ya wanyama hawa na kuwa kama jamii ya wanyama wanaofugwa.

Inafika hatu ngiri hata wanapofikia hatua ya kuzaa basi hulazimika kuingia kuzaa katika mazingira ya nyumba za watu au kwenye mabanda ya mbuzi na ng'ombe kitu ambacho hakitakiwi kabisa kwa upande wa wanyamapori kuwa na mahusiano na binadamu au wanyama wafugwa kwa kiasi hiki.

Siasa

# Rais Samia anavyozidi kuipaisha TIRDO

## ■ Kupima ngozi sasa ni hapa hapa nchini




Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO), Profesa Mkumbukwa Mtambo (mwenye suti ya bluu) akiwa na Mkurugenzi Mkuu wa REPOA, Dk. Donald Mmari wakisikiliza maelezo ya matumizi ya mashine za kupima ubora wa mkaa mbadala kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Nishati, Hossen Kayumba, katika maabara za shirika hilo.

**Na Hellen Mwango**

SAFARI za kwenda nje ya nchi kusaka maabara zinazotoa huduma za kupima kiwango cha ubora na matumizi sahihi ya ngozi, sasa zitakuwa historia, baada ya Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO), kupata maabara za kisasa na hivyo kupata suluhisho kwa wajasiriamali na wadau wa ngozi nchini.

Wajasiriamali na wadau wanaochakata ngozi walilazimika kutumia gharama kubwa kwenda nje ya nchi kupata huduma za kupima ubora wa malighafi hiyo lakini Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan imeliwezesha shirika hilo mashine za kisasa kwa ajili ya kuhudumia Watanzania.

Mkurugenzi Mkuu wa TIRDO, Profesa Mkumbukwa Mtambo alisema serikali inayoongozwa na Rais Dk. Samia imewawezesha mashine za kisasa na bado kuna nyingine ziko njiani na kilichaobaki ni wao kuwatumikia Watanzania.

"Mtaalam wa utafiti akishapata mashine za kukamilisha shughuli zake za utafiti, kazi yake ni kufanyakazi, sisi tulikuwa na shida ya mashine lakini sasa tumewezeshwa jukumu letu la kupima ubora wa ngozi ili kuwapunguzia wajasiriamali gharama ya kwenda kupata huduma hiyo nje, sasa inabaki kuwa historia, viwanda na taasisi za umma waje wapate huduma TIRDO," alisema.

Anasema Watanzania sasa wajivunie cha kwao, hakuna tena sababu ya kutumia gharama kubwa kusafirisha ngozi kwenda kupima nje, mashine zetu zina ubora wa hali ya juu, waje wapime ili kama kwenda nje bidhaa hiyo ianze kuuzwa katika masoko ya nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na masoko mengine ikiwa na nembo ya Tanzania.

Anasema kwa sasa shirika lake limeanza kufanyakazi na baadhi ya taasisi za serikali ikiwamo, Mkemia Mkuu wa Serikali, na linaanda mchakato wa kuingia makubaliano na Shirika la Viwango (TBS), ili wanapokamilisha tafiti zao hasa kwa vijana wapate vyeti vitakavyowatambulisha sehemu mbalimbali.

"Tunataka kuingia makubaliano na TBS ikiwamo kuwasaidia kufanya vipimo pamoja na kutoa vyeti kwa makundi mbalimbali hapa kwetu vitakavyowatambulisha katika shughuli zao," anasema Profesa Mtambo katika mahojiano yake na Uhuru Media Group ofisini kwake.

Akifafanua zaidi anasema, mashine hizo zina uwezo wa kutambua matumizi halisi ya ngozi kama ni kwa ajili ya viatu, mabegi, mikoba au vitambaa na kwa hiyo, Awamu ya Sita imejizatiti kumkomboa mjasiriamali.


Mkurugenzi wa Maendeleo ya Uhandisi TIRDO, Ramson Mwilangali, anaelezea majukumu makubwa na faida za shirika hilo kwa Watanzania.

Anasema TIRDO mbali na kufanya utafiti, pia inatoa ushirikiano mkubwa kwa viwanda vya hapa nchini na wajasiriamali lakini hawaishii hapo tu, wanatoa ushauri wa njia sahihi za kuwahamasisha waendelee kufanya shughuli zao za uzalishaji.

"Maabara ni nyenzo za utafiti na kuwasaidia wajasiriamali wanapata fursa ya kutambua kama bidhaa zao zina sifa zilizowekwa, ikitokea hazina sifa tunachukua jukumu la kutoa msaada ili wafikie sifa stahiki," anasema.

Anasema, maabara ya ngozi hapa nchini ni mkombozi kwa






wajasiriamali na wadau wa bidhaa hiyo, si tu inamsaidia kujua ubora wake, bali hata kujua matumizi yake.

"Ngozi zinatofautiana matumizi yake, huwezi kutumia ngozi ya kutengenezea kiatu, ukatengenezea mkoba au begi, kwa hiyo mashine zetu zinafanya utambuzi na kubaini matumizi halisi ya ngozi, wajasiriamali waje kupima, waje wapate huduma na kuthibitishiwa ubora hapa nchini," anasema na kuongeza.

"Tunawaasa wajasiriamali kuja kupima viwango vyenye ubora hapa TIRDO ikitokea wasiotimiza vigezo hawatarudi bila kupata elimu kwetu ikielekeza nini kifanyike, tunawakaribisha waje, wenye viwanda si wote wenye maabara za kuangalia uzalishaji tunawakaribisha," anasema.

Hata hivyo, anasema, Watanzania wakitumia maabara za TIRDO kutaondoa utoroshwaji wa ngozi kwenda nje kuchakata na kwamba inapotoroshwa haiwezi kutambulika kama ni mali ya Tanzania.

Anasema serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara, wanapata mashine na vifaa mbalimbali vinavyohitajika katika maabara yao na kwamba bado wana imani na Rais Dk. Samia na wanamatumaini ya kupata makubwa zaidi kutoka kwake.

Aidha anasema sasa serikali iwaangalie TIRDO kwa jicho la pili kwa upande wa rasilimali watu, iwaongezee wataalamu wa utafiti kutokana na uwezeshaji mkubwa ulifanywa na Rais.

"Sisi tunaiahidi serikali kufanyakazi stahiki kulingana na tulivyowezeshwa, tunasubiri wadau waje kupata huduma na uwezo wa kuwahudumia tunao," anasema Mwilangali.

Anafafanua kwamba shirika hilo, linalenga kuwajengea uwezo wa kuuza ngozi iliyotoka Tanzania moja kwa moja kwenda sokoni katika masoko ya nje ya nchi.

"Nina imani kuwa ajira zitaongezeka, uchumi utaongezeka na pato la taifa litaongezeka kupitia ngozi ya Tanzania," anasisitiza.

Naye Mtaalamu wa Utafiti wa Ngozi na Nguo, Bosco Mtweve anasema, mashine walizowezeshwa na Rais Dk. Samia baada ya kukaa muda mrefu bila vitendea kazi, zina uwezo wa kupima ngozi iliyochakatwa na ngozi mbichi iliyochakatwa kwa kutumia kemikali ili kuwa bidhaa ya ngozi kamili.

Pia mashine hizo zina uwezo wa kuangalia nguvu ya kemikali, kupoteza rangi, nguvu ya rangi na nguvu ya ngozi ikihifadhiwa kwenye joto.

Aidha anaeleza kuwa kemikali za kuchakata ngozi zikitumika vibaya zinaweza kusababisha madhara katika maghala ya kuhifadhiwa bidhaa hiyo.

"Kama ngozi nyingine zimeisha muda wake, zinapumua na kutanuka kwa hiyo wanaoathirika ni wale wanaotoa huduma katika ghala husika, pia kama zilichakatwa kwa ubora hafifu unasababisha ngozi yetu kuishia kupata soko la ndani kwa kuwa haiwezi kushindana kwenye la nje," anasema.

Anasma Watanzania wengi wanatamani kuuza nje ngozi ya hapa nyumbani lakini inakataliwa kutokana na wachakataji wetu kushindwa kufikia kiwango, sasa hilo limekwisha kwa sababu TIRDO imepata mwarobaini wa kupata ngozi yenye kiwango cha soko la nje," anasema.


Anafafanua kwamba kupitia mashine za shirika hilo wanatoa vipimo kwa wale wanaochakata ngozi mbichi iliyotumia kemikali na kutoa ushauri bora kwa wachakataji.

"TIRDO tunatoa mbinu mbadala kuendana na soko la dunia, wakija wadau hapa kwetu, kazi yetu kubwa ni kutoa elimu, mafunzo kwa wafugaji ikiwamo namna ya uchunaji sahihi kwa kutumia vifaa vya kisasa ili kupata ngozi bora kupitia njia nzuri za uchunaji," anasema.

Kuhusu wanyama wanaopigwa chapa, anasema si sahihi kufanya hivyo kwa kuwa ngozi inaharibiwa na hivyo kushusha thamani yake katika matumizi mbalimbali.

Anasema katika viwanda, ngozi inapokuwa na alama ya kupigwa chapa inalazimika kukatwa na kutupwa.

"Sisi hapa kwetu tunawashauri zile ngozi wanazotupa wanachafua mazingira tutawaelekeza namna ya kuzalisha bidhaa nyingine ikiwamo soli za viatu na kujiongezea kipato," anasema.



**Mtaalamu wa Utafiti wa ngozi na nguo, Bosco Mtweve aliendelea na kazi ya kupima ubora wa ngozi kutoka kwa wajasiriamali ili kupata matokeo halisi.**

Afya

# Makubaliano ya PPP yanavyoweza kuongeza kasi ya maendeleo barabara

Na Mwandishi Wetu

USHIRIKIANO kati ya sekta ya umma na binafsi (Public Private Partnerships-PPP), ni moja ya njia thabiti inayoweza kutumika kuleta mabadiliko katika sekta ya barabara.

Hii inatokana na ukweli kwamba maendeleo ya mtandao wa barabara kwa taifa lolote, ni muhimu katika kuchochea ukuaji biashara na kufanikisha uchumi wa kikanda.

Ushirikiano wa PPPs wenye faida, huvuta uwekezaji binafsi ambao hufanya kuwa chombo cha maendeleo ya haraka ya miundombinu.

Katika muktadha wa sekta ya barabara, PPP huongoza kwa kuboresha uunganisho wa mtandao na usafiri wa umma na kurahisisha biashara na uwekezaji.

Kimsingi, PPP inatarajiwa kusababisha ufanisi katika usafiri wa umma, biashara na uwekezaji ambao unalingana na adhma ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, anayesisitiza mageuzi katika sekta ya umma.

Kwa kuangalia jinsi nchi nyingine zilivyofanikiwa katika hili, unaweza kuchukuliwa mfano wa nchi kama Afrika Kusini ambapo zaidi ya miradi 300 ya PPP, imefanywa tangu mwaka 1994.

Kitengo cha Hazina ya Taifa ya Afrika Kusini (The South African National Treasury), chombo kinachoshughulikia miradi ya PPP, imeweka taratibu zilizothibitishwa katika kushughulikia miradi ya PPP ambayo inaongoza mchakato wa ushirikiano kati ya taasisi ya sekta ya umma na taasisi binafsi.

Chini ya mwongozo kama huo, taasisi binafsi zinachukua hatari (risks) kubwa ya kifedha, kiufundi na uendeshaji katika kubuni, ufadhili, ujenzi na uendeshaji wa mradi.

Taifa letu limekuwa likifadhili miundombinu kupitia fedha za umma ambazo zinakusanywa kwa njia mbalimbali iwe katika mifumo ya kodi au mikopo.

Historia inaonyesha kuwa sekta ya barabara imekuwa ikinufaika zaidi na fedha za umma. Walakini, kumekua na ongezeko la mahitaji ya kifedha kwenye miradi ya maendeleo ya barabara.

Hali hii imefikia hatua ya kuleta mzigo mkubwa kwa mapato ya nchi na kusababisha kasi duni katika sekta ya barabara.

Aidha, imekuwa ikujulikana kwamba hali duni ya barabara za umma, imeathiri nchi yetu tangu Uhuru. Kwa upungufu kama huo, tunalazimika kufikiria upya mbinu ya kukusanya uwekezaji wa mtaji kwa ajili ya maendeleo ya mtandao wa barabara.

Wakati ni jukumu la serikali kufadhili maendeleo ya miundombinu kupitia fedha za umma, mikataba ya PPP hutoa chaguo la kutekeleza miradi ya miundombinu ambayo mtaji wa awali unatolewa na sekta binafsi na chini ya muundo uliokubaliwa wa kandarasi.

Ni dhahiri kwamba upatikanaji wa fedha za sekta binafsi, unaruhusu uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya umma, na hii ni kwa sababu ufadhili wa umma kwa mara nyingi haupatikani kwa wakati kutokana na shinikizo linalosababishwa na mahitaji mengine katika sekta za kijamii.

Kwa sababu hii, inaongeza umuhimu zaidi kwa sekta binafsi katika kushirikiana na sekta ya umma katika ngazi mbalimbali za maamuzi nchini.

Sekta ya kilimo inayochangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wa Taifa, inategemea sana mtandao wa barabara ulio na uhakika na unapatikana kwa rahisi.

Uhusiano huu kati ya uzalishaji wa kilimo na hali ya mtandao wa barabara unaweka shinikizo kwa serikali kufadhili maendeleo na matengenezo ya miundombinu ya barabara.

Ili kupunguza shinikizo hili kwa serikali, njia za kisasa za ufadhili lazima ziwazwe, zitengenezwe na kutekelezwa kwa manufaa ya pamoja ya muda mrefu.

Takwimu za sasa zinaonyesha kuwa mtandao wa barabara chini ya mamlaka ya Tanroads unafikia kilomita 36,760 za barabara, ambapo kilomita 11,919 (asilimia 32) zimeboreshwa hadi viwango vya lami wakati kilomita 24,841 (asilimia 68) bado zinasubiri ufadhili wa kuboreshwa hadi viwango vya lami.

Katika hali ngumu kama hiyo na wakati huu wa kihistoria miaka 62 baada ya Uhuru, tunalazimika kufikiria na kurekebisha njia na mbinu za ufadhili wa miradi ya barabara kwa kuzingatia sana PPPs (ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi).

Ushirikiano wa PPPs unatarajiwa kuleta faida nyingi kwa nchi yetu, ikiwa ni pamoja na mambo yafuatayo: -

Udhamini wa kifedha

Inajulikana kwamba serikali yetu imekuwa ikikabiliwa na ufinyu wa ufadhili wa miradi ya barabara kwa muda mrefu.

Kwa kuanzishwa kwa PPPs, nchi yetu hatimaye itawaruhusu wawekezaji binafsi kuingiza mtaji, kupunguza mzigo kwenye fedha za umma na kuruhusu serikali kutenga fedha kwa sekta muhimu nyingine za kijamii kama afya, nishati vijijini, elimu, na usambazaji wa maji salama.

Uwekezaji wa miundombinu kwa ujumla huhitaji mtaji mkubwa katika awamu ya ujenzi na gharama zinapungua katika hatua za uendeshaji na matengenezo.

Kwa mfano kwenye PPPs, barabara au mabwawa ya umeme, kwa mfano, ni ghali kubuni na kujenga, lakini mara tu ujenzi unapokamilika, zinapunguza sana gharama za uendeshaji na matengenezo.

Inaendelea Uk. 15





**Inatoka Uk. 14**

Uboreshaji wa usafiri wa umma kupitia uwekezaji wa PPPs katika miundombinu, hasa barabara, uwezekano wa usafiri bora ni dhahiri.

Jamii zilizo mbali na zile ambazo hazijapata huduma vizuri zitanufaika zaidi. Kwa muhtasari, usafiri wa umma unachochea uchumi na hivyo kuboresha maisha ya jamii na taifa. Mwingiliano kati ya sekta na makundi ya aina zote, ikiwa ni pamoja na ile rasmi na isiyo rasmi, unaleta uhai katika ustawi wa kijamii.

Ufanisi na Ubora:-

Katika muktadha huu, PPPs mara nyingi huleta usimamizi bora wa miradi, ufanisi na ubora. Wakandarasi wenye utaalam katika ujenzi wa barabara na matengenezo, kwa mfano, wanaweza kuwasilisha teknolojia za kisasa na kuhakikisha kunakuwa na miundombinu iliyo na ubora wa hali ya juu.

Motisha muhimu zaidi ya matumizi ya PPPs kama njia mbadala ya ufadhili wa miundombinu, ni uwezekano wa kupata faida za muda mrefu.

Ni muhimu kuelewa kuwa unapotumia PPP kwa mradi wowote ulio kwenye mfumo na michakato sahihi, kuna faida nyingi zinazoweza kufikiwa.

Kwa PPPs, hupunguza gharama za muda mrefu kwa rasilimali za sekta ya umma. Hii ni hata baada ya kuzingatia gharama kubwa ya mtaji (gharama za kifedha) zinazohusiana na ufadhili wa kibinafsi unaokuwa sehemu ya PPP.

Kwa miradi ya PPP inayotumia mfumo wa malipo ya mtumiaji, ufanisi unaweza pia kusababisha malipo ya chini kwa watumiaji na uaminifu katika miundombinu ya usafiri.

Bila kujali njia ya mkataba, changamoto ya kiufundi (yaani, mradi) inapaswa kujaribiwa kupitia uchambuzi wa gharama na faida zake kwa kipindi cha muda mrefu.

Suluhisho pia lazima liwe na manufaa na thamani kwa matokeo ya kijamii na kiuchumi kwa kiwango kikubwa na kwa kipindi cha muda mrefu.

Ni kwa kuangalia muktadha huu mradi unapaswa kujaribiwa kama "unaofaa kwa PPP" kwa madhumuni ya kubainisha ikiwa utoaji wa PPP utatoa ufanisi unaotarajiwa.

Kuchochea ubunifu na mabadiliko

Aidha, kutokana na asili ya mabadiliko ya mikataba ya PPPs, kwa kiasi fulani huchochea ubunifu unaofanana na mkazo wa Rais Dk. Samia kwenye mageuzi na mikakati ya kujenga upya.

Katika muktadha huu, inaweza kusemwa kwamba wakati mahitaji katika mkataba wa PPP yanapoundwa kwa usahihi, huangalia zaidi ufanisi wa kiutendaji na matokeo yanayotarajiwa.

Kwa hiyo, uwezo wa sekta binafsi wa kubuni, utatoa chanzo cha ziada cha kutengeneza akiba na kuongeza ufanisi.

Maendeleo ya Rasilimali Watu kusimamia na kutekeleza miradi ya PPP, kutahitaji maendeleo ya ujuzi siyo tu kwenye shughuli za uhandisi bali pia katika utawala na usimamizi wa mikataba.

Kwa muktadha wa maendeleo ya rasilimali watu, mfumo wa ufadhili wa miradi ya PPP mara nyingi huwa na mchango wa moja kwa moja katika kutoa fursa za ajira.

Ni dhahiri kwamba kuna faida za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja mbalimbali zinazotokana na makubaliano ya PPP katika sekta zote za uchumi zilizounganishwa.

Umma unapaswa kuelimishwa ili kuelewa kwamba tuna mazingira mazuri ya kurekebisha na kujenga upya mfumo wa kufadhili miundombinu ya barabara.

Uungaji mkono kutoka kwa watu wa kila sehemu ya maisha, utatupeleka mbele ikiwa tunataka kukua pamoja kama taifa.

Uwezo wa serikali kufikia sekta zote kuhitaji msaada kutoka kwa njia nyingine za ufadhili kama PPP.

Ushahidi kutoka kwa nchi zilizoendelea kama Uturuki, Korea Kusini, Singapore, UAE n.k., juu ya mchango wa PPPs katika ufadhili wa miundombinu ni mkubwa na hatuwezi kusita tena.

Lazima tuondoe hali ya kutokuwa na uhakika, shaka na mtazamo wa kukata tamaa. Kila kitu kinawezekana chini ya jua ikiwa tuko tayari kwa mabadiliko na kuchukua hatua; hatua ambayo itakuwa mwanzo wa ustawi.

Ufadhili wa jadi umesaidia sana nchi yetu kustawi katika miaka ya hivi karibuni kwa kuongeza mtandao wa barabara na viwango bora vya barabara.

Hata hivyo, mafanikio haya lazima yapate msukumo zaidi kwa kutumia njia nyingine za ufadhili wa miradi kama PPP ili kuharakisha maendeleo.

Kwa vyovyote vile, maslahi ya umma lazima yalindwe ili kuhakikisha kuwa mali ya barabara chini ya PPP, inatumika kwa lengo lililokusudiwa na ndani ya mfumo wa kurejesha gharama.







Uchumi



# Teknolojia yavuta vijana kwenye ujenzi

**Na Claudia Kayombo, Singida**

FANI ya ufundi ujenzi au uashi, imekuwa ikitoa ajira nyingi nchini kwani majumba yaliyoko maeneo mbalimbali na barabara nadhifu ni kazi ya mafundi ujenzi.

Mafundi waaminifu ambao wanajenga majengo mbalimbali katika jamii ni nadra kukosa kazi kwani kila kukicha shughuli za ujenzi huendelea katika maeneo mbalimbali ikiwamo ujenzi wa makazi na hata vibanda vya biashara kwa maeneo ya pembezoni mwa miji.

Kwa maeneo ya mijini waashi hao ambao pia wanajenga shule, makanisa na misikiti, huko hujenga kumbi za starehe na majengo makubwa ya biashara zikiwamo ofisi.

Hata hivyo, si wanajamii wengi wanaofahamu iwapo ufundi ujenzi nao umegawanyika katika makundi mbalimbali.

Mwalimu Said Ali wa Idara ya Ujenzi katika Chuo cha Ufundi Stadi (VETA), mkoani Singida, anasema wapo wachora ramani za majengo, wajenzi wa majengo, wapo wasoma ramani na wasuka nondo lakini pia wapo wajenzi wa barabara na madaraja.

Anabainisha kuwa hao wote wanaitwa mafundi ujenzi ambao jamii inawategemea katika kuendelea sekta hiyo nchini kwa kiwango cha ufanisi mkubwa.

Mwalimu Ali anasema mchora ramani yeye anabobea katika kazi hiyo pekee, huku mjenzi naye akijenga jengo pamoja na mfumo wa maji taka, kuweka nakshi kuta na kumalizia kwa kuweka marumaru au saruji katika sakafu.

Hata hivyo, Mwalimu Ali anasema licha ya ufundi wa majengo kuwa na vipengele hivyo, lakini kwa yule ambaye atapenda kujifunza umaliziaji wa jengo pekee kwa maana ya kupaka rangi kuta na kuweka marumaru anaweza kufundishwa pia.

"Kutokana na mgawanyo huu hata wanawake nao wangejitokeza wangechagua kazi za kupaka rangi au kuweka marumaru, nimesema hivi kwa sababu wengi hufikiri ujenzi ni kazi ngumu na ni lazima kujenga majengo.

"Kupaka rangi au kuweka marumaru hakutumii nguvu, hata ujenzi wenyewe pia siku hizi hautumii nguvu, kutokana na kusambaa kwa teknolojia baada ya dunia kupiga hatua katika maendeleo ya sayansi na teknolojia, itafika wakati tofauti litainuliwa kwa nyezo badala ya nguvu," anasema.

Aidha, anabainisha kuwa aina nyingine ya mafundi ni wale wasuka nondo na wasoma ramani, wao kazi yao ni kusoma ramani na kusuka nondo zinazotumika katika ujenzi, huku mafundi ujenzi wengine ni wale wanaojenga barabara na madaraja.

Anasema chuo hicho kinapika mafundi bora wa ujenzi ambao baada ya kuhitimu huaminiwa na kuajiriwa katika maeneo mbalimbali ikiwamo serikalini na katika sekta binafsi huku wengine wakijiajiri wenyewe.

Anasema hata wale wanaojiajiri huishi maisha mazuri kwa kuwa jamii inakubali kazi nzuri wanazofanya baada ya chuo kuwaandaa vizuri ili kufanya kazi hiyo kwa ufanisi.

"Katika vyuo vinavyofanya vizuri kwenye sekta ya ujenzi na nyingine kama useremala, VETA Singida ni chuo cha kupigiwa mfano, wahitimu wake wanafanya vizuri maeneo mengi wanayoajiriwa au kujiajiri.

"Wanafunzi wetu wanapohitimu mwaka wa tatu, baadhi wanajiendeleza katika shtashahada wanakuwa walimu, wengine wanaajiriwa serikalini na wengine katika taasisi binafsi na wengine hujiajiri wenyewe," anasema mwalimu Ali.

Anabainisha kuwa wahitimu wengine wanajiunga na majeshi mbalimbali kwa maana ya JWTZ, Polisi, Magereza, Uhamiaji na hata Zimamoto na Uokoaji ambapo wanakwenda kutumia ujuzi walioupata kwa ufanisi mkubwa wawapo huko.

"Pia kampuni zinachukua wahitimu wetu wa miaka mitatu, yote hayo yanafanyika kwa sababu chuo chetu kinaaminiwa kwa ufundishaji wa mfano," anasema Mwalimu Ali.

Mwalimu huyo anaendelea, "Chuo chetu (VETA Singida) kina kampuni ya ujenzi, kupitia kampuni hiyo tunapewa tenda za kujenga katika maeneo mbalimbali.

"Kama chuo tunaalikwa kwenda kujenga katika maeneo mbalimbali nchini, mfano tumeshawahi kujenga jengo la Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), Sapiwi Simiyu.

"Pia vijana wetu wameshiriki katika ujenzi wa chuo kipya cha VETA Ikungi," anasema mwalimu Ali.

Anabainisha kuwa kampuni hiyo ya ujenzi ipo tayari kufanya kazi popote kwa viwango vizuri na kwa bei nafuu.

"Mtu au taasisi fulani ikitaka kujengewa jengo tupo tayari, aje chuoni azungumze na ofisi, tutafanyakazi yake vizuri," anasema.

Akibainisha changamoto inayoikumba idara hiyo ni uhaba wa wanafunzi wanaopenda kusomea fani ya ujenzi kwa ujumla.

Anatanabahisha kuwa licha ya mwitikio mdogo sana kwa wanawake wanaojitokeza kusomea ufundi huo, hata wanaume wanaojitokeza nao ni wachache.

Anasema hilo linatokana na jamii tangu miaka ya nyuma kuona fani hiyo inahitaji nguvu zaidi hivyo wengi wanapenda kufanya kazi lakini si za kutumia nguvu.

Anasema chuo hicho kipo mbioni kuanza mradi wa kufyatua tofauli imara ambazo zitauzwa kwa bei nafuu kuwawezesha wanaotaka kujenga kuwa na uhakika wa sehemu ya kuzipata.

Wakati mchakato huo ukiendelea, anasema idara yake inakabiliwa na changamoto nyingine ya uhaba wa vifaa vya kutengenezea tofali za urembo licha ya kuwa jambo hilo linafanyiwa kazi na menejimeti ya chuo hicho.

Mmoja wa wanafunzi wa mwaka wa tatu wa idara hiyo, Maro Mwita, anawataka vijana kuchangamkia kozi ya ufundi ujenzi kwani itawatoa kimaisha.

Anasema yeye amepata elimu nzuri tofauti na dhana aliyokuwa nayo kabla hajaanza masomo ambapo alikuwa anafikiri kuwa atajenga majengo pekee kumbe kuna vipengele vingi mno mwanafunzi anaposomea kozi hiyo na kwamba akibobea hata husika katika kushika tofali badala yake anakuwa msimamizi wa jengo husika.

"Ukiwa chuoni unajifunza mambo mengi sana yanayohusiana na ujenzi, unaweza ukawa unajenga huku ukafungua duka kubwa la vifaa vya ujenzi kwa kuwa utakuwa unavijua vifaa kuliko yule asiyepata elimu chuoni.

"Nina uhakika na maisha baada ya kuhitimu hapa, hata kama sitaajiriwa nitajiajiri kupitia ufundi wangu lakini pia nitatafuta mtaji ambapo nitafungua duka kubwa la vifa vya ujenzi ambapo wajenzi watakuwa wana uhakika na eneo la kupata vifaa mbalimbali kutoka katika duka langu," anasema.



Paul Mng'ong'o

## KLINIKI YA FIKRA

Simu: 0676055444 Email: mngongopaul@yahoo.com

# Tabia unazotakiwa kuziacha haraka usonge mbele

BAADHI ya watu, wana hulka ya kufanya mambo yao pasipo kuwa na mpangilio na hatma yake, kutofanikiwa kama walivyotarajia. Wanasaikolojia walifanya utafiti na kuibaini kuwa ni muhimu mambo yafuatayo kuzingatiwa kwa mtu mwenye malengo ya kutaka kusonga mbele kimaisha kwa mafanikio.

**1. Acha kupenda kuwaridhisha au kuwafurahisha watu.**

Hili ni tatizo kubwa kwa jamii yetu hususan jamii za kijamaa ambazo watu wanaishi kama ndugu. Watu wanapenda maoni ya watu na wanajaribu kumfanya kila mmoja aridhike. Ndiyo maana kwenye jamii hizi, wengi hawaendi mbali. Tabia hii itakufanya ujitahidi kufanya wanavyotaka watu na mwisho kujikuta uko kama zao. Tabia hii inakuondolea upekee wako ambayo ni moja ya siri kubwa za kufanikiwa. Ukitaka kusonga mbele, hakikisha wazo lako, lipime kwa vipimo sahihi kisha jiamini na usonge mbele

**2. Acha kujilinganisha na wengine.**

Kwenye maisha, unahitaji kufanya tofauti ili kupata matokeo tofauti. Ukitaka kujilinganisha na wengine, tegemea matokeo waliyoyapata.

**3. Acha kujishtukia**

Ukiamua kufanya jambo, anza hatua za kufanya, acha kujishtukia na kujiona kama huwezi. Jambo la msingi ni kuhakikisha kuwa wazo lako ni sahihi. Hakuna siku utajiona unaweza, unachotakiwa ni kuanza kisha katika safari unajenga uwezo. Wote wanaofanya makubwa, kuna siku waliamua na kuanza na ukiwauliza, watakwambia kuwa uwezo wao umeendelea kujengeka siku baada ya siku.

**4. Acha kukimbia changamoto**

Vikwazo ni sehemu ya safari. Tafuta jinsi ya kutatua na si kukimbia. Hakuna kisicho na changamoto. Hata ukiamua kulala siku mbili, utapata changamoto tu ya kuumwa mbavu. Usikimbie changamoto kabiliana nazo kwa kutafuta njia na kuzitatua.

**5. Acha kujidanganya/ kujiridhisha**

Mara zote tafuta uhalisia ili ukupe njia sahihi. Usichukulie mambo kirahisi. Hakika njia zako bila kudharau wala kuchukulia poa. Kwa lugha rahisi hapa nasisitiza uwe makini na ufanye mambo kwa tahadhari na kumaanisha hata kama unachofanya ni kidogo.

**6. Acha kufanya kawaida (ili mradi)**

Mara zote fanya kwa ubunifu, maarifa na ustadi. Tambua chochote kisichokuuma hakitawagusa wengine. Ukifanya mambo kiholela, matokeo yake ni holela pia. Unapofanya jambo, tuliza akili, kuwa mbunifu, jiulize maswali mengi, wekeza nguvu ili upate kilicho bora.

**7. Kutofanya maandalizi ya kina Jiandae vizuri kwa kila kilicho mbele yako.**

Maandalizi mazuri yanakupa urahisi na manufaa makubwa kwenye kulifanya jambo. Mfano mchezo wa dakika 90 wa mpira, unaweza kuandaliwa mwezi mzima. Mchezo wa ngumi wa round nane, huandaliwa miezi mitatu au zaidi.

Hapa nakuonesha umuhimu wa kujiandaa na kitu unachokifanya.

**8. Acha visingizio**

"Ukihitaji jambo utatafuta njia, lakini kama hutaki, utatafuta visingizio". Hakuna kushindwa kunakokosa visingizio. Ukitaka kufanikiwa, acha kutafuta visingizio. Kiri kushindwa na uangalie nini kilikufanya ushindwe kisha amua kuwa hutashindwa tena.



**9. Acha Ubinafsi**

Njia yako inahitaji watu sahihi ambao una nafasi kwao nao wana nafasi kwako. Watu wanaweza kuwa sababu ya uimara wako au sababu ya anguko lako. Pamoja na angalizo hilo, bado ukweli ni kwamba unahitaji watu ili kusonga mbele. Unachotakiwa kufanya ni mambo mawili makubwa, acha ubinafsi na uchague watu sahihi.

**10. Acha kulalamika sana**

Tabia hiyo inakufanya ujioneshe dhaifu usiye na uwezo wa kubadili hali ila unataka huruma za watu.

**11. Acha kukosoa kila kitu Jifunze kuona mema zaidi kuliko mabaya**

Huwezi kupata kitu usichokiona mara kwa mara. Ukiwa kila wakati unaona ubaya na kukosoa, hatuwezi kutegemea matokeo mema kwako. Badili mtazamo, kulalamika sana ni zao la mtazamo hasi.

**12. Acha tabia ya kuahirisha mambo.**

Tabia hii inaweza kuwa moja kati ya tabia chache kubwa zinazowafanya wengi kutopiga hatua. Jiulize unapanga mambo mangapi na unatekeleza mangapi? Utagundua hata wewe ni mhanga na mwathirika wa ugonjwa huu mkubwa wa kuahirisha mambo.

**13. Kutaka kuwa sahihi wakati wote**

Ni mhimu sana kuhakikisha kuwa unakuwa sahihi, lakini kuacha kufanya mambo kwa ajili ya kutafuta usahihi tu kutakuchelewesha sana.

**14. Acha tabia ya kusema "Ndiyo" hata mahali ambapo ulitakiwa kusema "Hapana".**

Watu wengi hdhani kusema ndiyo ni unyenyekevu au busara.

Jambo la kwanza ni vizuri kila siku uwe na ratiba ya mambo ya kufanya. Kama wewe una ratiba yako ya mambo ya kufanya, halafu kikija kitu kingine hutakubali kila kitu ili kutekeleza ratiba yako. Ndiyo yako iwe ndiyo kama una nafasi na kama huwezi au huna nafasi sema hapana.

**15. Acha mawazo (mtazamo) hasi Yaani kuona kushindwa tu.**

Ni vizuri kuwa na muda kujiuliza wewe unaona nini kwenye maisha. Huwezi kupata matokeo usiyoyaona kwenye mtazamo kwanza. Kama kuna vitu vya kuviacha kwa haraka, ni mtazamo hasi.

**16. Acha kupuuza malengo yako na kutoka kwenye njia.**


Siku zote timiza malengo usitoke kwenye lengo lako wala kuacha njia yako.

**17. Acha kuwa na mtazamo wa pesa kuliko matokeo ya kuleta suluhu ya tatizo kwenye jamii.**

Wazo lako ni vizuri ukilipanga kwa kuangalia matokeo yake chanya kwenye kuwahudumia watu au kutatua tatizo fulani kwenye jamii. Wazo lolote linalolenga kutatua tatizo kwenye jamii, litainuliwa kwa gharama yoyote. Lakini mpango ukilenga fedha, inaweza kukusumbua.

Kama ungependa kupata ushauri au usimamizi wa karibu katika kuishi mwongozo huu, (unaweza kuwa taasisi, kikundi, kanisa, umoja, Ngo au mtu binafsi), karibu sana tutashirikiana nawe kwa neema na msaada wa Mungu.

**MWENYEZI MUNGU TUNAKUOMBA DUA UMPE MAISHA MAREFU, AFYA NJEMA, NGUVU ZAIDI NA MAFANIKIO ,,RAIS WETU MPENDWA DK. SAMIA SULUHU HASSAN**



# Miili 44 ajali ya moto bado haijatambuliwa



**JOHANNESBURG, Afrika Kusini**


ZAIDI ya nusu ya waathiriwa wa moto wa Agosti 31, mwaka huu ulioteketeza jengo lililotekwa nyara katika jiji la Johannesburg, Afrika Kusini bado hawajajulikana.

Idara ya Afya ya Gauteng ilisema imewatambua waathiriwa 18 zaidi pamoja na wale 12 wa awali na kufanya jumla ya miili ambayo utambulisho wao umefahamika kufikia 30.

Motalatale Modiba, Msemaji wa Idara ya Afya ya Gauteng, alisema miili ya ziada ilitambuliwa kupitia uchunguzi wa kidijitali wa alama za vidole zilizookolewa za waathiriwa na uchunguzi wa miili na wanafamilia wao.

Hata hivyo, Modiba alifichua kuwa miili 44 kati ya jumla ya 77 iliyopatikana kutokana na moto bado haijatambuliwa.

Aliviambia vyombo vya habari kuwa kwa sasa wanafanya uchanganuzi wa DNA kwenye miili 38 kati ya 44 iliyosalia ili kufichua utambulisho wao na manusura 27 bado wanatibiwa hospitalini. *BBC.*



# Ujerumani ‘yaipiga jeki’ Ukraine



**BERLIN, Ujerumani**

UJERUMANI imeahidi kuipatia Ukraine msaada ziada wa kiutu wa kiasi cha Dola milioni 21, lakini imezuia kutoa msimamo wa wazi juu ya iwapo itaipatia Ukraine makombora ya masafa marefu aina ya Taurus.

Tangazo la msaada huo wa nyongeza lilitolewa na Waziri wa Mambo ya Kigeni wa Ujerumani, Annalena Baerbock, aliye ziarani nchini Ukraine baada ya kukutana na mwenzake wa Ukraine, Dmytro Kuleba.

Kuhusu suala la makombora ya Taurus, Baerbock alisema Ujerumani bado haijafikia uamuzi wa kutuma makombora hayo yenye uwezo mkubwa na asingeweza kutoa ahadi kabla ya muafaka kupatikana, msimamo ambao yumkini haukumfurahisha waziri mwenzake wa Ukraine ambaye ameirai Ujerumani kutopoteza wakati:

“Tungekuwa tumepata mafanikio zaidi na kunusuru maisha ya wanajeshi wa Ukraine na raia kama tungekuwa tumepata makombora ya Taurus. Tunaiambia serikali ya Ujerumani kwamba tunaheshimu majadiliano yenu lakini kwa tunachofahamu hakuna msingi wowote hadi sasa wa kupinga kutupatia silaha hizo,” alisema.

Ukraine inaamini makombora hayo ya Taurus yataiwezesha kuvikabili kwa uzani ulio sawa vikosi vya Urusi vilivyoivamia nchi hiyo Februari mwaka jana. *DW*

# Mnangagwa apingwa kuteua mwanawe, mpwawe

**HARARE, Zimbabwe**

RAIS wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa, ameshutumiwa kwa upendeleo baada ya kumteua mwanawe katika Baraza jipya la Mawaziri kufuatia kuchaguliwa tena katika uchaguzi mwezi uliopita.

Mnangagwa Jumatatu alimtaja mwanawe, David Kudakwashe, kama Naibu Waziri wa Fedha kama sehemu ya mgawo wa vijana katika Bunge.

Pia alimteua mpwa wake, Tongai Mnangagwa kuwa Naibu



Waziri wa Utalii, vyombo vya habari vya ndani viliripoti.

Mthuli Ncube, mfanyakazi wa zamani wa benki, alibaki kama Waziri wa Fedha huku Mwenyekiti wa Kitaifa wa Chama tawala cha Zanu-PF, Oppah Muchinguri-Kashiri, akiteuliwa tena kuwa Waziri wa Ulinzi.

Mbunge wa chama kikuu cha upinzani cha Citizens Coalition for Change (CCC), Fadzayi Mahere, amemshutumu Rais Mnangagwa kwa kuchochea upendeleo.

Hayakupatikana majibu rasmi kutoka kwa Chama Tawala au Rais juu ya tuhuma hiyo. Hata hivyo, wafuasi wa Mnangagwa wanasema mwanawe amestahili kuwania nafasi hiyo.

Kuchaguliwa tena kwa Mnangagwa kumepingwa na upinzani ukitaja madai ya udanganyifu, huku baadhi ya waangalizi wakisema kuwa kura hiyo haikukidhi viwango vya kikanda na kimataifa. *BBC.*

# UN yataka kurejeshwa demokrasia Niger, Gabon

**NEW YORK, Marekani**

MKUU wa Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa, Volker Turk, ametoa mwito wa kurejeshwa haraka utawala wa kiraia kwenye mataifa ya Afrika yaliyoshuhudia mapinduzi ya kijeshi.

Volker alisema mwenendo wa kuchukua madaraka kwa nguvu, siyo suluhu kwa matatizo yaliyopo.



Katika hotuba yake mbele ya mkutano wa Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa, Volker alisema njia pekee kuyashughulikia matatizo ni kuwa na utawala wa kiraia unaotoa nafasi kwa umma kuwa huru kuikosoa serikali na kushinikiza mageuzi.

Alizungumzia pia athari za mabadiliko ya tabianchi na ukosefu wa huduma muhimu akisema ndiyo yanachangia hali ya kukata tamaa miongoni mwa raia duniani na kuchochea hisia za itikadi kali.

Hotuba hiyo ya jumla imemulika vilevile mizozo ya wakimbizi tangu Myanmar, huko Mexico na hata nchini Mali.

Ukosefu wa usalama nchini Haiti na ukandamizaji wa makundi ya walio wachache ulimwenguni, ni sehemu ya masuala mengi yaliyoorodheshwa na mkuu huyo wa haki za binadamu kama changamoto zinazoikabili dunia. *BBC*

# Marekani sasa kuweka vikwazo vipya



**WASHNGTON DC, Marekani**

MSEMAJI wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani, Matthew Miller, amewaambia waandishi wa habari Jumatatu kwamba Marekani iko tayari kuweka vikwazo vipya ikiwa Vladimir Putin na Kim Jong-un watakubaliana kuhusu usambazaji wa silaha za Korea katika mkutano huko Vladivostok.

“Ningependa kuzikumbusha nchi zote mbili kwamba uhamishaji wowote wa silaha kutoka Korea Kaskazini hadi Urusi, utakuwa ukiukaji wa maazimio mengi ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Na, bila shaka, tumetekeleza kikamilifu vikwazo dhidi ya watu binafsi wanaofadhili vita vya Urusi, tutaendelea kuvitekeleza, na hatutasita kuweka vikwazo vipya ikibidi,” alisema Miller.

Marekani inaamini kwamba Urusi ingependa kupokea silaha kutoka Korea Kaskazini, hasa mizinga.

Miller alisema katika taarifa kwamba Putin, “anasafiri katika nchi yake nzima kumwomba Kim Jong-un msaada wa kijeshi.” BBC.

# CRDB, NMB sasa Tunahitaji Kombe la Taifa

Na Petter Mwendapole

TIMU ya soka ya Taifa ya Tanzania 'Taifa Stars' imefuzu kwenda katika fainali za kuwania ubingwa wa Mataifa ya Afrika.

Hii ni mara ya tatu kwa Tanzania kupata nafasi hiyo muhimu ambayo imekuwa ndoto ya wachezaji na watanzania wote kwa ujumla.

Tanzania imekata tiketi katika hali ambayo kama ilikuwa ikipumulia mashine.

Wakati matokeo ya Stars yakionekana kukera wengi, mpaka kuamsha hoja za kuzidi kwa wachezaji wa kigeni ndio sababu za mkwamo wa timu hiyo, lakini bado imeweza kuvuka.

Hamasa ya Rais Samia Suluhu katika michezo, ndio ilikuwepo wakati timu hiyo ikifuzu

Mwaka 2009, wakati wa utawala wa Rais Jakaya Mrisho Kikwete. Rais Kikwete alichangia kuletwa kwa Kocha Maxio Maximo, akawezesha timu kuweka kambi kule Brazil.

Wakati huo Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania alikuwa mchezaji wa zamani wa timu za Yanga, Pan African na Taifa Stars, Mhandisi Leodeger Chilla Tenga.

Huyu alikuwepo kwenye kikosi kilichokwenda fainali za AFCON mwaka 1980. Tanzania ikaenda kwenye fainali za CHAN, (Wachezaji wanaocheza mashidano ya ndani) yaliyofanyika huko Ivory Coast na Congo kuwa mabingwa wa kwanza.

Kwa sasa Tenga ndio Mwenyekiti wa Baraza la Michezo Tanzania (BMT). Mwaka 2019, Taifa Stars ilikwenda tena AFCON chini ya Kocha Emmanuel Amunike japo hatukufanya vizuri.

Ni kweli tumefuzu, tukiwa peke yetu kwenye ukanda wa Afrika Masharuki, jirani zetu Zambia na Congo wao kwenda AFCON sio habari, wapo pia mwaka huu.

Tumeomba kuandaa mashindano yajayo ya AFCON tukishirikiana na Kenya, Uganda, tumenza kuandaa viwanja, tumeanza kufanya michezo mashuleni kuwa sehemu kamili ya mtaala wa masomo.

Mipango mizuri sana, kwa baadae, lakini hawa walioko mashuleni sasa iwe sekonfldari au msingi hatuwezi kuwaandaa kwa ajili ya timu ya miaka minne ijayo, kwa vyovyote watakuwa hawajakomaa.

Kama haitoshi macho yetu yanaangalia zaidi uchaguzi wa wachezaji wale wanaowika katika klabu zetu za Simba, Yanga sana siku hizi Coastal Union, Azam na Singida. Hawa makinda hawatakuwa na nafasi katika vikosi hivyo.

Pengine huu ni wakati sahihi wa kurudisha michuano ya Kombe la Taifa.

Turudishe ule mfumo kila mchezaji wa mkoa fulani arudi kuchezea timu ya kwao, hii itasaidia hata wachezaji walioko kwenye timu za mqdaraja mengine huko mikoani wakapata nafasi, kwenye timu hizo.

Hii itasaidia kutengeneza timu imara ya Taifa, kwa maana makocha wa mikoa watakuwa na muda mrefu wa kuangalia wachezaji huko kwao na baada ya kuweka kambi, timu itakapoingia kwenye mashindano itakuwa imewiva.

Mashindano haya yatumike na benki kama CRDB ama NMB kuyadhamini kwa maana wao wana mizizi mirefu huko mikoani.

Udhamini wa benki hizo kwenye mashindano hayo, utaondoa zile kelele za kugombea wachezaji kupitia shindano linalodhaminiwa na taasisi shindani.

Kimsingi Kombe la Taifa ndio ambalo linashirikisha nchi nzima kwa wakati mmoja, tofauti na Ligi Kuu ambayo haina uwakilishi wa timu kutoka kila mkoa.

Huku mikoani wako hawa kina Aziz Ki wengi zaidi, wapo kina Cletous Chama wengi zaidi ni kwa vile hawajapata jukwaa sahihi la kuonekana.

Kama ambavyo kina Tenga waliweza kutokea Umiseta ni wazi kwenye kombe la Taifa tutawapata wengine.

Kilio chetu cha washambuliaji kitatatuliwa na mashindano ya aina hii.

Badala ya kupigana vita ni bora tuangalie fursa zingine ambazo matokeo yakitokea nasi tunasema ni sehemu ya ushindi huo.

Kama nia ni kujenga hatuna haja ya kugombea fito, tunapaswa kuunganisha nguvu, tunapaswa kuanza sasa. Ninaupenda wimbo wa Twanga Pepeta usemao, Kumekucha, jua la chomoza, wiki, mwezi, mwaka, siku zenda mbio hazirudi nyuma na ukitaka kuanza maisha anza sasa usisubiri Kesho. Huu ndio wakati sahihi wa Kombe la Taifa



**Kwa sasa Tenga ndio Mwenyekiti wa Baraza la Michezo Tanzania (BMT). Mwaka 2019, Taifa Stars ilikwenda tena AFCON chini ya Kocha Emmanuel Amunike japo hatukufanya vizuri.**

# Hamza Kalala asimamie kuirudisha Vijana Jazz

**Na Ibrahim Mkamba**

UZOEFU unaonesha kwamba bendi ya muziki ikitoa nyimbo kali kali, ujue haina muda mrefu itatoweka. Album kali ya Music Clarification ya Empire Bakuba, Inde Monie ya Kanda Bongoman, Beyoni na Noel Confiance za Bozi Boziana ni miongoni mwa mifano michache.

Sikinde walienda huko kileleni na album za Pata Potea 1982, Mandela 1983 na Hiba 1984. Mungu mkubwa waliendelea kutamba sana mpaka leo wapo lakini kule walikuwa kileleni mno. Msondo nao walikuwa juu mno na Kilio cha Mtu Mzima 2003 kisha Piga ua Talaka Utatoa 2004 lakini Mwenyezi Mungu mkubwa mpaka leo wanakiwasha kweli kweli.

Vijana Jazz walitisha mno kwenye lile toleo la Ogopa Tapeli, Azza, Wivu, Penzi Haligawanyiki na Mama wa Kambo ni Mama. Hapo walikuwa juu sana. Walijitahidi mno baada ya mhimili wao Hemed Manety kufariki mwaka 1990 kuifanya bendi isimame na ilisimama na kina Jerry Nashon, Suleiman Mbwembwe, Mohammed Gotagota na wengine lakini kwa sababu kadhaa, ikiwemo vifo vya wanamuziki, bendi ikaenda chini kidogo kidogo na mpaka sasa haijulikani kama ipo au imekufa.

Ukweli ni kwamba bendi ya Vijana Jazz ni nembo kubwa ya Umoja wa Vijana wa CCM na ni moja ya taasisi zenye kupendwa mno na Watanzania wote wa itikadi mbali mbali. Bendi hii inapaswa irudishwe juu kama iko chini au ifufuliwe kama imekufa.

Anayeweza kuirudisha bendi hiyo kiuhakika ni mwanamuziki Hamza Kalala akishirikiana na kila aliye hai aliyepita kwenye bendi hiyo kama George Mpupua, Beno Villa Anthony, Cosmas Chidumule na wengine kwa njia ya mikakati na kushauriana. La msingi, mmiliki atafute vyombo vya muziki na ajenge nia ya kuirudisha juu bendi hiyo.

Sababu za kumpendekeza Hamza Kalala kwa hilo ni hizi zifuatazo. Kwanza, bendi hiyo kwa Hamza Kalala ni kama nyumbani. Alikuwemo ndani ya bendi hiyo kwa vipindi vingi tofauti kuanzia miaka ya mwanzo mpaka miaka ya Ogopa Tapeli. Alienda huku na kule lakini kituo kikuu kilikuwa Vijana Jazz.

Sikumbuki album ambayo Kalala alikuwemo Vijana Jazz ambamo hakutunga wimbo. 1982 Cosmas akiwemo na nyimbo zake tatu; Nilitaka Iwe Siri Yetu, Unikubalie na Maisha ni Safari Ndefu huku Manety akiwa na Jiko Limenuna, Kalala alitoa Kiapo (Unachotenda Kiapo, kwa kweli siyo sahihi we bwana umtendeapo wema mtoto wa (... kike, usijaribu ulipwe ujira wa mapenzi bali asante (masaksafoni). Mimi Dora nasumbuka, katika kuhangaika huku na kule, kazi ofisini mwako zataka watu...)

Mwaka 1983 mwanzoni kwenye Maisha ya Amba wa Hemedy Manety, Hamza Kalala aliibuka na Zenaba. Baadaye mwaka huo 1983 Jerry Nashon alipoibuka kwa mara ya kwanza akitunga nyimbo nyingi, Kalala akatoa wimbo Penzi Halina Umaarufu maarufu kama Midabwada. 1984 wakati wa Mzee Tupatupa, Kalala alitunga wimbo Stella akimuelezea mchumba wake binti wa Mzee John Momose Cheyo.

Miaka michache kabla hajafariki, Abuu Semhando aliuzungumzia wimbo huo kwa kusema kwamba alishiriki kupiga drums kwenye wimbo huo katika kushiriki kumzungumzia huyo shemeji yake Stella. Akasema Kalala na Stella wakaoana na kujaaliwa watoto ambapo mtoto wao Kalala Junior alikua na kuwa mwanamuziki aliyeshirikiana naye kwenye bendi moja, mtoto wao huyo akiimba yeye Semhando akipiga drums!

Mwaka1985 Vijana Jazz walikuja na Mary Maria ya Hemedy Manety ambapo Kalala aliibuka na Ilikuwa Lift tu. 1987 kwenye Magaidi wa Msumbiji na Nivunje Kikombe Nisivunje, Kalala aliibuka na wimbo Na Nani kisichokuwa na thamani kwako wee bwana kwa Mungu kina thamani ee. Wewe ukisema mke gani we bwana wenzio wanamuona anapeendeza....).Mwaka 1988 kwenye nyimbo zile zilizotajwa, alitunga Mama wa Kambo ni Mama.

Sababu nyingine kwa nini Hamza Kalala anafaa kuifufua Vijana Jazz ni uwezo wake mkubwa wa kufanya kazi na vijana. Nilisikia Umoja wa Vijana wa CCM unataka bendi yao iwe na sura ya ujana kwa maana ya kuwa na wanamuziki vijana. Kalala amefanya kazi kubwa na nzuri na vijana wadogo wengi kwenye bendi ya Bantu Group.

Kuna story moja ya kusisimua ya mwaka 1993 kule Shinyanga nilipokuwa na nyota moja nikiwa ofisi ya CID Shinyanga chini ya OC-CID kaka yangu Marehemu Exaud Mushi, apumzike kwa amani na OCD Mzee wangu Marehemu Ringo, apumzike kwa amani.

Wanamuziki kadhaa, vijana wadogo mno mwaka huo kina Ally Choki walileta kituoni kwa tuhuma ya kum-baka msichana mmoja aliyelewa sana aliyekuwa akicheza muziki wao kwenye ukumbi mmoja uitwao Bimbo wa eneo la Ngokolo hapo Shinyanga. Ukweli yule binti hakubakwa bali alijitahidi kujilengesha kwa wanamuziki vijana wadogo hao lakini wao hawakuwa na habari naye.

Kalala alipofika kituoni kufuatilia kesi hiyo, nikajitambulisha kwake kwamba hata mimi nilishwahi kuwa mwanamuziki (haikuwa kweli, niliishia kwenye upenzi wa muziki) nikamwambia nilishangaa vitoto vyake kubaka wakati wanamuziki hawabaki bali hupapatikiwa na wanawake.

Tulipokuwa kwa OCD nikiwa na mkuu wangu OC-CID pamoja na Hamza Kalala, aliwaambia viongozi wangu kwa lafudhi yake ya kikongo, "huyu (akinionesha) zamani alikuwa muzishian. Yeye iko najua muzishianz hatubaki wanawake ila wanawake wanatupapatikia."

Sikutoka kwenye mstari huo, nikawaambia hivyo viongozi wangu, wakaelekeza binti ahojiwe vizuri na tulipomhoji vizuri alikiri kudanganya na kuomba radhi ndipo vitoto, vikina Ally Choki vikawa huru.

Kalala akanikaribisha onesho lililofuata hapo hapo Shinyanga. Nilipohudhuria onesho hilo nilishangaa sana kuona vijana wadogo sana walivyokuwa wakipiga muziki mkubwa mno wa Kasimbago Kaabuka.

Umoja wa Vijana wa CCM utafute vyombo vipya, umkabidhi Hamza Kalala airudishe Vijana Jazz ya vijana. Kalala akipata shavu hilo, atengeneze timu ya wazee wote waliopo waliopitia Vijana Jazz. Vichwa vyao vitairudisha kiuhakika bendi hiyo pendwa sana. Asanteni.



# Everton matatani kupigwa bei



**LIVERPOOL, England**

KLABU ya Everton ambao ni wasumbufu wa Premier League wanakaribia kuuzwa kwa kampuni ya uwekezaji ya 777 Partners yenye makao yake Miami.

The Toffees walioathirika kifedha walianza tena mazungumzo na kampuni ya Marekani baada ya mazungumzo na MSP Sports Capital baada ya kuvunjika mwezi Agosti.

Utwaaji huo utamaliza umiliki wa msukosuko wa mmiliki Farhad Moshiri, ambaye aliwekeza kwa mara ya kwanza mnamo 2016. Chanzo kilicho karibu na Moshiri kilisema Everton wametafuta uwekezaji kwa muda, lakini mpango huo bado haujakamilika.

Kikosi cha Sean Dyche kiko katika nafasi ya 18 kwenye msimamo wa ligi baada ya kuambulia pointi moja pekee kutoka kwa mechi nne za kwanza walizocheza hadi sasa msimu huu.

Everton wako katika hali mbaya ndani na nje ya uwanja, wakiponea chupuchupu kushuka daraja katika misimu miwili iliyopita, ikiwa ni pamoja na kusalia na ushindi katika siku ya mwisho muhula uliopita.

Mwezi ujao klabu hiyo itaenda mbele ya tume huru kwa madai ya ukiukaji wa sheria za haki za kifedha za Ligi ya Premia, lakini Everton wamekanusha makosa hayo na kusema "wako tayari kutetea kwa dhati" msimamo wao.Mnamo Machi, klabu ilichapisha hasara za kifedha kwa mwaka wa tano mfululizo, na kupelekea hasara zao katika kipindi cha miaka mitano iliyopita hadi zaidi ya paundi milioni 430.

Pia wako katika harakati za kujenga uwanja mpya kwenye Bramley Moore Dock na gharama inaweza kufikia paundi milioni 760, ongezeko la paundi milioni 260 kutokana na takwimu zilizonukuliwa na klabu hiyo mwaka jana.

# The Ben kutumbuiza Bujumbura



**BUJUMBURA, Burundi**

Nyota wa muziki wa R & B kutoka Rwanda, Benjamin Mugisha, maarufu kwa jina la The Ben, anatarajiwa kutumbuiza kwa mara ya kwanza mjini Bujumbura, Burundi.

Ben ana mashabiki wengi zaidi nchini Burundi na anatarajiwa kufanya onyesho Oktoba Mosi.

Msanii huyo anayeishi Marekani, kwa sasa anatamba na kibao chake Why ndio msanii anayelipwa zaidi nchini Rwanda.

Mara kadhaa msanii amekuwa akipata mialiko kutumbuiza nchini Burundi lakini amekuwa akishindwa kuafikiana na waandaji kutokana na kutofika dau alilotaka.

Imeelezwa kuwa msanii huyo amelipwa kiasi cha Faranga 45,000 sawa na sh milioni 87 za Kitanzania kwa sjoo moja.

# Pogba asimamishwa




**TURIN, Italia**

KIUNGO wa kati wa Juventus ,Paul Pogba (30) amesimamishwa kutocheza kwa muda kwa kosa la kutumia dawa za kusisimua misuli.

Kiungo huyo alyeijiunga tena na Juventus kwa uhamisho wa bure Julai 2022 baada ya mkataba wake kumalizika Manchester United, alipewa mkataba wa miaka minne kuitumikia timu hiyo.

Uongozi wa Juventus umesema umechukua hatua hiyo kutokana matokeo ya vipimo vya madawa yaliyochukuliwa kwa wachezaji, wakati wa mechi baina ya kikosi chao na Udinese ambapo majibu yaliyoonyesha mshambuliaji huyo anatumia dawa.

Tangu kurejea kwaTurin, Pogba amekumbwa na majeraha ya mara kwa mara ambayo yalimfanya kukosa fainali za Kombe la Dunia mwaka jana nchini Qatar.

Hivi majuzi, kocha wa Juventus, Massimo Allegri akisema mchezaji huyo alipata tatizo dogo la mgongo wakati wa mechi dhidi ya Empoli.

Pogba alikutwa na hatia hiyo kutokana na uchunguzi uliofanyika baada ya mechi japo alikuwa kama mchezaji wa akiba.

Mshambuliaji huyo ambaye hakutumiwi alichaguliwa kwa bahati nasibu kwa uchunguzi wa dawa za kulevya.

Na Iwapo atapatikana na hatia ya kutumia dawa za kusisimua misuli, anaweza kupigwa marufuku kati ya miaka miwili na minne.

# Phodeni anafaa pembeni

**LONDON, England**




KOCHA wa timu ya Taifa ya England, Gareth Southgate amesema mshambuliaji Phil Foden ana uwezo mkubwa wa kucheza pembeni badala ya katikati anapofikiria kuhamia.

Mwanasoka huyo anayeichezea, Manchester City mapema mwezi Machi mwaka huu alisema kuwa ilikuwa nafasi ambayo alitaka kuhamia katika miaka michache ijayo katika majukumu ya timu yake ya taifa na kila mara amekuwa akijiona kucheza na kufanya vizuri kwenye nafasi hiyo.

Foden, mwenye umri wa miaka 23, ametumiwa katika nafasi ya kiungo wa kati na Kocha wa City Pep Guardiola.



# Singida wafungulia geti Jumapili

Inatoka Uk. 24

Katika pambano hilo, Singida wamewataka mashabiki kwenda uwanjani hapo na jezi za timu tatu zinazoshiriki mashindano ya kimataifa, ikwemo yao, Yanga na Simba.

Msemaji wa timu ya Singida, Hussein Masanza alisema lengo la hamasa hiyo ni kuhakikisha inatia moyo wachezaji wao ili waweze kuvuka katika hatua hiyo na kwenda katika hatua ya 16 bora ya michuano hiyo.

Uongozi wa timu hiyo, umeandaa jezi maalumu kwa ajili ya viongozi wakuu wa nchi na watafikishiwa ili kuleta umoja wa kitaifa.

Viongozi hao ni pamoja na Mh.Dkt.Samia suluhu hassan, Makamu wa Raisi Dkt. Philip Mpango, Waziri Mkuu Kasimu Majaliwa, Raisi wa Zanziba Dkt. Hussein Mwinyi na Naibu Waziri Mkuu Dkt. Dotto Biteko.

Maofisa wa Habari na Mawasiliano wa klabu za Yanga, Simba na Azam walikuwepo katika mkutano huo ili kutimiza kauli ya Rais, Dk. Samia Suluhu kutaka timu zinaposhiriki mashidano ya kimataifa kushirikiana badala ya kuombeana mabaya.




# Wavu wamaliza kwa ushindi

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Taifa ya mpira wa Wavu ya wanaume, Almas King imemaliza mashindano ya Mataifa ya Afrika yanayofanyika nchini Misri kwa ushindi dhidi ya Burundi.

Ushindi huo haukuweza kuivusha Almas kwenda kwenye nusu fainali lakini umeipandisha viwango vya mchezo huo Afrika. Katika mchezo huo, Almas walishinda kwa seti 3-1.

Almas sasa wameshika nafasi ya 13 kwa ubora wa wavu Afrika. Katika mechi ya jana, Almas walishinda seti ya kwanza kwa walishinda kwa pointi 22-20, seti ya pili Burundi wakarudi na kishindo cha pointi 25-22.

Seti ya tatu Almas waliamka na kuibuka na ushindi wa pointi, 25-20 kabla ya kumaliza seti ya mwisho kwa pointi 25-16.

Timu hiyo ambayo ilikutana na Balozi wa Tanzania nchini Misri inatarajiwa kurejea nchini kesho ambapo wachezaji watarejea katika timu zao ili kujiandaa na mashindano ya ligi ya mchezo huo.

# Mwakinyo, ziwekwe dola pambano na Kiduku

**Na Mwandishi Wetu**



BONDIA wa kimataifa wa Tanzania, Hassan Mwakinyo amesema hana mpinzani katika wanamasumbwi wa Tanzania na endapo Twaha Kiduku anataka kupambana nae promota aweke dola za maana.

Katika mkutano na waandishi wa habari, Mwakinyo amesema kwa kupigana na bondia wa Tanzania kwa sasa hakumuongezei chochote kwenye viwango vya ubora wa ndondi duniani.

“Mi sina mpinzani Tanzania, lakini kuna mtoto wa Morogoro yeye anapoiga kilele na kuomba sana kuoigana nami aendelee kuomba, huenda akafanikiwa.

“Ikiwa heri na maombi yamejibiwa, huyo promota ajiandae kwa hela ya maana, lazima atoe dola, na pambano limeisha kuna nyumba ziko pale inabaki kumbukumbu, apartment zile lilikuwa pambano la Mwakinyo na yule mtoto wa Morogoro,” alisema.

Mwakinyo anatarajia kupambana na bondia kutoka nchini Kenya, Rayton Okwiri. Alisema kwa sasa hana anachoweza kupata kwa mabondia wa Tanzania zaidi ya fedha labda.

# Twiga Stars kamili kwa Ivory Coast

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI kaka zao, Taifa Stars wakiwa wamefuzu kwenda Ivory Coast hapo mwakani kwa michuano ya Mataifa ya Afrika (AFCON), kikosi cha wanawake, Twiga Stars kiko kambini kujinoa kwa michuano kama hiyo.

Meneja Uhusiano wa Shirikisho la Soka TanzaniA (TFF) Clinford Ndimbo alisema timu iko kambini katika kituo cha shirikisho kilichopo Kigamboni, Dar es Salaam kujiandaa na mechi yake na Ivory Coast.

“Mpaka sasa hakuna taarifa za majeruhi, kila kitu kinaenda vizuri kwa usimamizi wa makocha wao, wachezaji wako kwenye ari ya juu kuhakikisha wanashinda mechi hiyo muhimu.

“Hamasa imeongezeka zaidi baada ya matokeo ya Taifa Stars kwenda AFCON lakini pia kitendo cha Jeshi Stars kutwaa Ubingwa wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA) na kukata



tiketi ya kucheza klabu bingwa ya Afrika,” alisema.

Kikosi hicho kiko chini ya kocha Bakari Shime ambapo mechi ya mwisho, Twiga ilicheza na Uganda katika mechi ya kirafiki na kufungwa mabao 3-1.



# Paul Pogba asimamishwa Juventus

Uk. 22

Leo yetu ndiyo kesho yetu

Uelekeo Spoti

| Jumatano Septemba 13 - 19, 2023|



# Singida wafungulia geti Jumapili

**Na Wemael Mmaraba.**

TIMU ya soka ya Singida Fountain Gate imetangaza kuondoa kiingilio katika pambano lao la raundi ya pili ya michuano ya Kombe la Shirikisho Barani Afrika dhidi ya Future ya Misri.

Inaendelea Uk. 23

# Kigali tayari kimewaka

**Na Karangwa Clarine, Kigali**

WAKATI Yanga wakiendelea kujipanga kwenda Kigali Rwanda na mabasi 50 sawa na watu 3250 kwenda nchini humo, El Marreikh wana mpango pambano hilo kuchezwa bila mashabiki.

Yanga na El Marreikh wanapambana kuwania tiketi ya kucheza 16 bora ya michuano ya Klabu Bingwa Afrika. Marreikh wanatumia Uwanja wa Pele, Kigali kama Uwanja wao wa nyumbani, kutokana na Sudan kuwa na machafuko.

Habari kutoka nchini humo zinasema El Marreikh kwa upande mmoja wanataka kulipia gharama za mchezo huo ili kuzuia msafara wa klabu ya Yanga ambao wao ndio watakuwa wametawala Uwanja huo.

Marreikh juzi walianza utaratibu wa kuzuia mashabiki kuangalia mazoezi yao ili kutotoa siri za kambi yao.

Hata hivyo Shirikisho la Soka la Rwanda (FERWAFA) lilikuwa linafanya mazungumzo na El Marreikh juu ya suala hilo ikiwa Rwanda wanataka kutangaza uwanja wao kwa ajili ya jumuiya ya kimataifa, hjivyo kuzuia mashabiki hakuisaidii Rwanda.

Meneja Habari na Uhusiano wa Yanga, Ally Kamwe yeye alisema tayari suala hilo limekwisha na kwamba tiketi za mzunguko zitauzwa kwa sh 13,000 za Tanzania.

Awali Rwanda walikuwa na uwanja wa Amahoro ambao ndio ulikuwa ukitumika kwa mashindano mbalimbali ya kimataifa.

Mwisho wa mashabiki kujiandikisha kwenye mabasi ni leo, wakati juzi Yanga walizindua kampeni nyingine ya wanaotaka kusafiri kwa ndege na sambamba na timu watalipa dola 900 za Kimarekani.





# ...Pilato anatoka Madagascar

**Na Mwandishi Wetu, Kigali**

Shirikisho la mpira wa miguu barani Afrika (CAF) limemtangaza refa, Andofetra Rakotojaona raia wa Madagascar kusimama katikati kwneye mechi ya Yanga na Eli Marreikh ya Sudan.

Mechi hiyo inafanyika Jumamosi kwenye Uwanja wa Pele mjini Kigali, Rwanda.

Andofetra atasaidiwa na waamuzi wa pembeni Lionel Andrian na Augustin Herinirina huku kamishna wa mchezo huo akiwa ni Amir Abdi Hassan.

# Twiga Stars kamili



Uk. 23



Uk. 23

# Mwakinyo: Ziwekwe dola tu pambano na Kiduku